# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

## KWA MWAKA 2021/2022

**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHE. ABDULLA HUSSEIN KOMBO (MBM) WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

**MEI, 2021**

YALIYOMO UKURASA

UTANGULIZI....................................................................................1
MUELEKEO WA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR....................4
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2020/2021.........................................................................10
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021..............................................................................11
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA SHABAHA ZA PROGRAMU ZA WIZARA YAUCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021..............................................................................13
PROGARAMU YA MAENDELEO YA UVUVI.............................13
Programu ndogo ya maendeleo ya uvuvi na uhifadhi wa bahari.......13
Programu ndogo ya ufugaji wa mazao ya baharini..........................16
Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini..........................18
Kampuni ya Uvuvi Zanzibar – ZAFICO..........................................19
PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU........22
Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA)..............................................................................23
Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (ZPDC).............26
PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA WIZARA...............................................................................29
Programu ndogo ya Mipango na Usimamizi wa kazi za Wizara.......30
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji...................................32
Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba..................34
CHANGAMOTO..............................................................................35
HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO..............................................................................36
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021 /2022.................................................................................................38
MAKADIRIO YA MATUMIZI 2021/2022....................................38

MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022..........................................40
MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA 2021/2022..........................................................................................42
PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU........47
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu.....................47
Mamlaka ya Udhibiti waUtafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar..........................................................................................48
Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar................50
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI...........................51
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Bahari; ..........................................................................................52
Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini...............................54
Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari.......................55
Kampuni ya Uvuvi ZAFICO...............................................................57
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI..............................................58
Programu ndogo ya utawala na uendeshaji.........................................59
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti.......................................60
Programu ndogo ya uratibu wa kazi za Wizara Pemba.......................61
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.............................62
HITIMISHO..........................................................................................63
VIAMBATANISHO.................................................................................66
Kiambatanisho Nam. 1a: Uzalishaji wa Samaki (Tani).........................67
Kiambatanisho Nam. 1b: Usafirishaji wa Mazao Baharini (Tani).......68
Kiambatanisho Nam. 2: Jadweli la Upatikanaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/21..........................................................................69
Kiambatanisho Nam. 3: Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2020- Machi 2021.....................................................70
Kiambatanisho Nam. 4: Jadweli la Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo Julai 2020 hadi Machi 2021................................................71
Kiambatanisho Nam. 5: Mchanganuo wa Makadirio na Matumizi kwa Kipindi cha Julai – Machi 2021 (ZAFICO)..........................................72

Kiambatanisho Nam. 6: Jadweli la Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka 2021/ 2022.........................................................73
Kiambatanisho Nam. 7: Jadweli la Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Kazi za Kawaida kwa Mwaka 2021/2022.........................................74
Kiambatanisho Nam. 8: Jadweli la Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka 2021/2022..................................................76
Kiambatanisho Nam. 9A: Mradi wa Usimamizi wa shughuli za Uvuvi wa kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOfish).....77
Kiambatanisho Nam. 9 B: Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki Malindi..........................................................................................80
Kiambatanisho Nam. 9 C: Mradi kutototolea Vifaranga vya Samaki, Kaa na Majongoo bahari (Marine Hatchery).......................................83
Kiambatisho Nam 9D: Mradi wa Kuimarisha Uvuvi na Kilimo (IFAD)...........................................................................................85
Kiambatisho Nam. 9E: Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa........................................................................................87
Kiambatisho Nam 9F: Mradi wa Kuanzisha Mashamba na Kufuga Samaki.........................................................................................88
Kiambatisho Nam 9G: Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Usarifu na Uhifadhi wa Bidhaa za Samaki ZAFICO.............................................89

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kazi za Kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

3. **Mheshimiwa Spika,** shukurani za pekee zimuendee Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupata ushindi mkubwa kupitia Uchaguzi Mkuu wa Octoba 2020. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu na uwezo wa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya umoja, usalama, amani na utulivu. Aidha, tunampongeza Mhe. Rais kwa kutoa miongozo na kusimamia vyema utekelezaji wa malengo ya ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka

2020 - 2025. Utekelezaji huu unaweza kufikia malengo yaliyowekwa kwa zaidi ya asilimia mia moja na mafanikio yatakayopatikana yataisaidia kwa kiasi kikubwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta maendeleo ya Sekta za Uchumi wa Buluu na Uvuvi sambamba na kuongeza tija kwa wananchi na kukuza uchumi wa nchi.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mama Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya Tanzania na kwa Afrika ya Mashariki. Aidha, tunamuombea dua kwa Mwenyezi Mungu ampe nguvu, uwezo na maarifa ya kuliongoza Taifa hili ili liendelee kuimarika kiuchumi na kufikia malengo yanayokusudiwa.

5. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Tunaamini kuwa viongozi hawa wakuu watamsaidia na kumshauri vizuri Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufikia azma yake ya kuboresha uchumi na maisha ya Wazanzibari. Vile vile, shukurani pia ziende kwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa Mawaziri na kumshauri Mheshimiwa Rais kufanya maamuzi mema na

kutumia hekima na busara kubwa katika kuleta maendeleo na kulinda haki za wananchi wote.

6. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii pia kukupongeza kwa dhati wewe mwenyewe kwa umakini na umahiri wako wa kuliendesha Baraza la Wawakilishi. Pia nawapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuteuliwa kushika nafasi hizo. Pia nawapongeza wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa kwao na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

7. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii adhimu kutoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Shaaban Ali Othman - Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi pamoja na Wajumbe wote na Sekretarieti ya Kamati hio kwa miongozo na ushauri waliotoa kwa Wizara katika kufanikisha vizuri utekelezaji wa shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2020/2021 na kutusaidia kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022. Napenda kuihakikishia kamati hio tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo mliyotupatia yamezingatiwa katika ukamilishaji wa bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatoa pole kwa watanzania wote kwa vifo vya viongozi wetu wapendwa, aliyekuwa Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; na

aliyekuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad. Mungu awalaze mahali panapostahiki Ameen.

## MUELEKEO WA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

9. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar, kama ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, tunawajibika kutekeleza maazimio na malengo ya Umoja wa Mataifa (Lengo Nam. 14) ya Uhifadhi wa bahari, na wajibu wa kushirikiana kwa pamoja kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha mafanikio ya uhifadhi wa bahari yetu ndani ya dhana ya Uchumi wa Buluu hususan katika maeneo ya sekta ya Uvuvi wa ndani na Bahari Kuu, Usafiri na Usafirishaji, Utafutaji wa Mafuta na Gesi na Ulinzi na Usalama Baharini.

10. **Mheshimiwa Spika,** Dhana ya Uchumi wa Buluu Zanzibar inajumuisha matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake pamoja na uhifadhi wa mazingira kwa maendelo ya kijamii na kiuchumi. Hivyo, Sekta ya Uchumi wa Buluu Zanzibar inajumuisha sekta za kiuchumi zinazohusiana na Maliasili za baharini na ukanda wa pwani. Sekta hizo ni pamoja na Uvuvi mdogo mdogo wa bahari ya ndani, Uvuvi wa Bahari Kuu, Kilimo bahari, ufugaji wa mazao ya baharini, usafiri wa baharini ikiwa ni pamoja na huduma za biashara na usalama katika usafirishaji baharini, Miundombinu ya kimkakati na viwanda katika huduma za bandari, Utalii wa Baharini na fukwe, Nishati mbadala na Utafutaji wa madini na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya uchumi wa Buluu na Uvuvi imeanza kutekeleza kwa vitendo kwa kufuata miongozo ya Dira ya maendeleo ya Zanzibar ya 2050 ambayo imetoa mwelekeo wa kimkakati wa kuratibu na kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetayarisha Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2021 pamoja na rasimu ya mpango mkakati wa Uchumi wa Buluu kwa lengo la kutekeleza malengo ya Dira ya maendeleo ya Zanzibar ya 2050 ili kusimamia ukuaji wa uchumi wa Zanzibar na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

12. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa vipaumbele vya Sera ya uchumi wa Buluu ya mwaka 2021 vitawezesha kuleta maendeleo ya Kiuchumi, na Kijamii katika harakati za kupunguza umasikini Zanzibar. Vipaumbele hivyo ni pamoja na: (i) Uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini; (ii) Usafiri na Usafirishaji Baharini pamoja na kuendeleza miundombinu na huduma za bandari; (iii) Matumizi endelevu ya nishati mbadala ikiwemo Mafuta na Gesi Asilia; (iv) Maendeleo ya Utalii; na (v) Uratibu wa utawala na Mazingira ya baharini “Maritime Governance”.

13. **Mheshimiwa Spika;** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane imekusudia kupambana na changamoto zenye kuzuia matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake kwa lengo la kukuza uchumi na kuondosha umasikini. Changamoto hizo ni pamoja na uvuvi haramu,

mabadiliko ya tabia nchi, usalama wa baharini na uharibifu wa mazingira ya bahari ikiwemo Matumbawe, Mikoko na Nyasi za Bahari. Aidha, katika kuendeleza juhudi za kupambana na umasikini, Wizara inategemea kutatua changamoto nyengine zinazokwaza maendeleo ya Uchumi wa Buluu kwa wananchi kwa kuwapatia mitaji yenye masharti nafuu, kuwajengea uwezo wananchi katika kuzitumia fursa zipatikanazo katika uchumi wa Buluu ikiwemo kuwapatia masoko na uongezaji wa thamani ya mazao ya baharini.

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya uchumi wa Buluu na Uvuvi imejipanga kushirikiana na taasisi mbali mbali za kitaifa, kikanda na kimataifa katika kuratibu na kusimamia matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake na kudhibiti uharibifu wowote ule wa maliasili zetu. Hii ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mikataba na maazimio ya kikanda na Kimataifa ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeyaridhia ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs), Mkakati wa Africa "Integrated Maritime Strategy", pamoja na Mkataba wa Lome wa Usalama wa Usafiri wa Baharini wa Umoja wa Afrika (AU). Pia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na Mabadiliko ya Tabia Nchi (UNFCCC), Mkataba wa Usimamizi na Uhifadhi wa Maliasili za Pwani na Baharini za Ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi chini ya Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Kamisheni ya Uvuvi wa Jodari katika Bahari ya Hindi iliyo chini ya Shirika la Chakula Duniani (FAO) na

Umoja wa Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi (Indian Ocean Rim Association).

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, katika kuhakikisha utekelezaji wa ahadi za kutengeneza ajira kwa wananchi wa Zanzibar chini ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM inazingatia matakwa ya maendeleo endelevu ya vizazi vya leo na kesho, uhakika na usalama wa chakula, kutekeleza mikakati ya kuondoa umaskini, kuinua hali za maisha na vipato vya wananchi pamoja na haki za jamii za ushiriki wao kikamilifu katika Uchumi wa Buluu. Wizara pia imeazimia kuendelea na juhudi zake za uhifadhi wa mazingira ya bahari yetu na kuendelea na mabadiliko ya tabia nchi yanayoiathiri bahari yetu kwa mujibu wa misingi ya utekelezaji wa Lengo Namba 14 la Umoja wa Mataifa la uhifadhi na usimamizi wa maliasili za bahari. Halikadhalika, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeazimia kushajiisha matumizi ya teknologia endelevu ya kisasa katika juhudi za kuwaongezea wananchi uwezo wa uzalishaji wenye tija na unaohifadhi mazingira katika sekta ya Uchumi wa Buluu. Aidha, Wizara itaratibu na kusimamia uundwaji wa Mamlaka yenye Uwezo (Competent Authority) na maabara ya kuthibitisha (certified laboratory) kwa lengo la kuwawezesha wajasiriamali wa Uvuvi, wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini kuweza kuzalisha bidhaa zenye ubora zitakazokidhi viwango (Standards) vya masoko ya ndani na nje ya nchi.

16. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ya Uchumi wa Buluu yanategemea sana kuwepo kwa Mpango Mahsusi wa Matumizi ya Bahari (Marine Spartial Planning). Hivyo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imepanga kushirikiana na wadau wote katika kuratibu na kushiriki katika utayarishaji na utekelezaji wa Mpango wa Matumizi ya Bahari. Mpango huo utawezesha kusimamia uhifadhi bora na thabiti wa bahari, kuvutia uwekezaji katika uvuvi, usafiri baharini, miundo mbinu ya bandari na uvuvi, utalii, nishati, mafuta na gesi, na kupunguza migogoro ya matumizi ya maeneo ya bahari na fukwe. Hivyo, kupitia mpango huo kutakua na mgawanyo mzuri wa maeneo ya wavuvi, wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini ikiwemo samaki, majongoo bahari na kaa. Aidha, Wizara itahakikisha maeneo ambayo tayari yametengwa kwa ajili ya shughuli nyengine za maendeleo ikiwemo utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia yanasimamiwa na kuendelezwa kwa kazi hizo kwa ufanisi mkubwa.

17. **Mheshimiwa Spika,** Mchango wa sekta ndogo ya Uvuvi katika pato la Taifa imechangia asilimia 4.8 kwa mwaka wa 2019. Aidha, mchango wa Sekta ya uvuvi kwa thamani ya pato la Taifa umeongezeka kutoka TZS190 Bilioni kwa mwaka wa 2018 hadi kufikia TZS 198 Bilioni kwa mwaka 2019. Aidha, uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tani 36,728 mwaka 2019 hadi tani 38,107 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Hata hivyo, Usafirishaji wa mazao ya baharini ikiwemo majongoo bahari, kaa na

pweza umepungua kutoka tani 20,845.3 mwaka 2019 hadi tani 12,167 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 41.6 **(Kiambatanisho Nam. 1A)**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda zinaendelea na utafiti wa mwani aina ya Glacelaria na kuhamasisha kilimo cha mwani aina ya Cottonii kwa kuongeza uzalishaji na usarifu wa zao hilo. Hata hivyo, usafirishaji wa mwani umepungua kutoka tani 11,204 mwaka 2019 hadi tani 8,967 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 19.97 **(Kiambatanisho Nam. 1B)** Kiujumla upungufu wa usafirishaji wa mazao ya baharini umesababishwa na kuwepo kwa mripuko wa maradhi ya COVID 19 yaliyoathiri shughuli za biashara duniani.

**19.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, Wizara imefanikiwa katika uendeshaji wa Programu 71 za kujenga uelewa kwa wananchi kupitia makongamano, mikutano ya shehia, Taasisi za Serikali na za kiraia pamoja na vyombo vya habari vikiwemo televisheni, magazeti na redio. Sambamba na hilo, sekta hii imefanikiwa kuandaa miongozo ya kisekta kwa ajili ya shughuli za Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imefanikiwa kukamilisha hatua za awali kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Uchukuaji wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia kwa Pamoja

"Multi – Client Seismic Survey" kwa eneo la Mashariki ya bahari ya Zanzibar sambamba na kuimarisha mfumo wa uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia.

21. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo ya Utangulizi sasa naomba uniruhusu niwasilishe utekelezaji wa programu za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2020/2021.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2020/2021

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imetekeleza malengo yake kupitia Programu Kuu tatu ambazo ni:

i. Maendeleo ya Uchumi wa Buluu.
ii. Maendeleo ya Uvuvi.
iii. Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

23. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia programu hizo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inasimamia utekelezaji wa Miradi mitatu (3) ya maendeleo ambayo ni Mradi wa Usimamizi wa Kazi za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Mashariki ya Bahari ya Hindi - SWIOFish, Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindi na Mradi wa Kutotolea Vifaranga vya Samaki.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Mipango Mikakati ya Kisekta. Utekelezaji wa Mikakati na Malengo hayo kumepelekea kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini. Aidha, mikakati hiyo imesaidia kujenga uelewa kwa taasisi za Serikali na sekta binafsi pamoja na wananchi kwa ujumla kuhusu kazi na biashara ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

**25.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Wizara ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 2.26 Bilioni** kutoka vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba ikiwa ni pamoja na Uvuvi wa Bahari kuu. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi, 2021, Wizara imekusanya jumla ya **TZS 547 milioni** sawa na asilimia 24 ya makadirio **(Kiambatisho Nam 2).**

**26.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliidhinishiwa kutumia **TZS 47.62 bilioni** kwa kazi za kawaida na kazi za Maendeleo.

27. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni **TZS 4.73 bilioni** ambazo ni sawa na asilimia **9** kati ya fedha hizo **(TZS 709.44 milioni** Mishahara na **91.18 milioni** kwa Matumizi mengineyo na **TZS 786.61 milioni** RUZUKU kutoka SMZ ambapo T**ZS 46.34 milioni** ni kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, **TZS 740.27 milioni** ni kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Uchimbaji na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) **(Kiambatisho 3)**. Kwa upande wa fedha za Maendeleo Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeingiziwa jumla ya **TZS 3.149 bilioni.**

Aidha, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia iliidhinishiwa **TZS 4.28 bilioni,** hadi kufikia machi, 2021 Kampuni imeingiziwa jumla ya **TZS 1 bilioni** ambazo ni Mtaji zikiwa ni asilimia 16 kwa fedha zilizopangwa kwa kipindi cha miezi tisa.

28. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ilipangiwa kutumia TZS 3.69 bilioni na imetumia TZS 1.43 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 39.

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA SHABAHA ZA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

29. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2020/2021, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilitekeleza programu zake za maendeleo ya Uchumi wa Buluu, maendeleo ya Uvuvi na programu ya uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI

30. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini. Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari na Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini.

### Programu ndogo ya maendeleo ya uvuvi na uhifadhi wa bahari

31. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari imelenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na uhifadhi wa bahari. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

i. Ujenzi wa Diko na Soko la samaki Malindi umefikia asilimia 30. Ujenzi huo umechelewa kukamilika kutokana na kuzuka kwa Janga la COVID 19, ambapo tarehe 2 April, 2020, Ubalozi wa Japani kupitia JICA uliwataka wakandarasi pamoja na washauri elekezi (wataalamu) ambao ni raia wa Japani na wanaotekeleza miradi inayopata misaada ya Serikali ya Japani kurudi nchini mwao. Hata hivyo wakandarasi hao tayari wamesharudi nchini na wanaendelea na ujenzi ambao unatarajiwa kukamilika mwezi wa Aprili 2022.
ii. Ujenzi wa Jengo la Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Rasilimali za Baharini pamoja na Maabara zake umekamilika.
iii. Ununuzi wa sanduku za barafu (ice box) 20 kwa ajili ya kuhifadhia barafu katika soko la Tumbe, Mkoani na Malindi umekamilika na tayari sanduku za barafu10 zimeshapelekwa Pemba na 10 zipo Unguja. Vilevile, Wizara inaendelea na ufungaji wa mashine za kutengenezea barafu katika Soko la Mkoani na Malindi.
iv. Doria shirikishi 154 zilifanyika kati ya doria 174 zilizopangwa katika maeneo ya hifadhi za MENAI, MIMCA na PECCA kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu (Nyavu za macho madogo, bunduki na madema ya waya) unaopelekea uharibifu wa mazingira ya bahari pamoja na kuangalia leseni za vyombo na wavuvi. Aidha, kutokana na doria hizo, matokeo 21 (11 Unguja na 10 Pemba) yaliyohusiana

na uvuvi haramu yameripotiwa vituo vya polisi na mashauri yao yamehukumiwa nje ya mahakama kwa kutozwa faini ya jumla ya TZS 18,900,000.

v. Kamati 22 zilipata mafunzo ya uchoraji wa ramani ya hali ya mazingira na matumizi ya rasilimali za bahari kwa lengo la kufanya usimamizi shirikishi katika maeneo yanayowazunguka ili waweze kuinua kipato chao pamoja na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya bahari ili kuongeza mazalia ya samaki.

vi. Zoezi la kukusanya taarifa za uvuvi (sensa ya uvuvi), ikiwemo vyombo, mitego, mwani pamoja na ufugaji wa samaki lilifanyika kwa lengo la kupata taarifa za uhakika zinazohusiana na uvuvi kwa ujumla na hivi sasa ripoti iko katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, zoezi la ufungaji na ufunguaji wa pweza limefanyika katika eneo la Michamvi kwa Unguja na Pujini kwa Pemba. Vile vile, Mafunzo juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya bahari na athari za uvuvi haramu yalifanyika ambapo jumla ya wavuvi 120 kutoka katika hifadhi za MENAI (45), MIMCA (40) na PECCA (35) walishiriki.

vii. Jumla ya wafanyakazi wanne (4) kati ya 8 waliopangwa wamepatiwa fursa ya mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali hapa nchini, ambapo wafanyakazi watatu wanaendelea na masomo katika ngazi ya shahada ya kwanza na mmoja anasomea shahada ya pili.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Programu ndogo hii iliombewa **TZS 39.99 bilioni** (**TZS 769 milioni** ni mishahara, **TZS 153.41 milioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, **TZS 39.06 bilioni** kwa ajili ya fedha za Maendeleo (**TZS 3.47 bilioni** kutoka SMZ na **TZS 35.59 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2021 Programu imepata jumla ya **TZS 3.76 bilioni** (**TZS 590.34 milion**i mishahara, **TZS 26.68 milioni** kwa kazi za kawaida. **TZS 3.14 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Kiambatisho 4) sawa na asilimia **9.6** na asilimia **12.5** kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

## Programu ndogo ya ufugaji wa mazao ya baharini

33. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini inalenga kuwahudumia wavuvi, wafugaji wa samaki, wakulima wa mwani na wadau wengine tofauti wanaojishughulisha na mazao mengine ya baharini. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

i. Jumla ya wafugaji 180 wa majongoo kutoka katika mikoa mitano kwa Unguja na Pemba walipata mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya mbinu bora za ufugaji wa majongoo bahari, pamoja na ujenzi wa vizimba vinne (4) vya mashamba ya mfano vyenye mita za mraba 1,800 kwa kila kimoja vilijengwa katika bahari ya vijiji vya Mkokotoni, Kama, Shungi - Makunduchi na Chwaka.

ii. Ziara ya kuangalia maeneo tengefu kwa ajili ya ufugaji wa vifaranga vya Majongoo ilifanyika katika vijiji vya Bungi na Kikungwi ambapo maeneo yenye upatikanaji mkubwa wa vifaranga vya Majongoo baada ya kukaguliwa na kupata ridhaa ya wananchi yaliwekewa mipaka na yalifungwa kufanya shughuli zozote za uvuvi ili kuhifadhi vifaranga na kuweka muda maalum wa kuvigawa vifaranga hivyo kwa wafugaji.

iii. Jumla ya samaki mama 132 wa sato na 21 kambare wamenunuliwa na kulelewa kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga. Jumla ya vifaranga 16,364 aina ya kambare na 12,970 aina ya sato vimezalishwa na kugaiwa kwa wananchi. Hata hivyo kwa sasa Wizara imeamua kukiendeleza kituo hicho cha kutotolesha vifaranga kwa njia ya ubia (PPP) ambapo tayari kuna hatua za awali za hati za mashirikiano zimefikiwa na baina ya Serikali na wabia wa Kampuni ya AGTEK (T) LIMITED & SHAZAIN FISHERIES LIMITED zikisubiri hatua ya kufanya upembuzi yakinifu.

iv. Jumla ya vijiji 14 (Unguja 9 na Pemba 5) vya wakulima wa mwani vimetembelewa na maafisa wa Idara ya uvuvi kwa ajili ya kufuatilia ukuaji, kusikiliza changamoto na kutoa elimu inayohusiana na kilimo cha mwani. Aidha, jumuiya ya kujenga uwezo wanawake (FAWE) imetoa mafunzo kwa vikundi 400 (250 Pemba na 150 Unguja) vya wakulima wa mwani. Vilevile, jumla ya vihori 500

(Unguja 200 na Pemba 300) walipatiwa wakulima wa mwani kwa ajili ya kuwasaidia katika shughuli zao za uvunaji wa mwani.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Programu hii ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini iliombewa TZS 153.4 milioni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2021 programu imepata TZS 25.58 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 17 ya fedha zilizoombwa na asilimia 23 kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

## Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini imetekeleza shabaha zifuatazo:

    i. Rasimu ya kitabu chenye taarifa za tafiti 1,016 za Uvuvi na Mazao ya Baharini zilizofanyika Zanzibar kuanzia mwaka 1999-2020 kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi imekamilika;
    ii. Mashirikiano na Washirika wa maendeleo (WIOMSA, KOICA na Benki ya Dunia) kwa taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na mazao ya Baharini) kuhusu matayarisho ya miradi yamefanyika.
    iii. Tafiti mpya ya mwani aina ya Glacilaria katika maeneo ya Fumba na Nyamanzi ipo katika hatua ya pili ya utekelezaji.

iv. Kukamilisha majaribio ya uzalishaji wa vifaranga vya majongoo bahari katika maeneo ya Bwachi kwa vijiji vya Bungi na Kikungwi ambapo jumla ya vifaranga 153,900 vimepatikana na kugaiwa kwa wafugaji.
v. Kukamilisha kipindi cha hali halisi ya ukulima wa majongoo Zanzibar kwa ajili ya utoaji wa elimu kwa jamii.

**36.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini iliombewa jumla ya **TZS 272 milioni** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2021 Taasisi imepata **TZS 46.34 milioni** kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 17 ya fedha zilizoombwa na asilimia 24 kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

## Kampuni ya Uvuvi Zanzibar – ZAFICO

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Kampuni ya Uvuvi **ya ZAFICO** ni kuanzisha Uvuvi wa kibiashara kwa kuimarisha ujenzi wa Miundombinu ya Uvuvi na kuelekeza nchi katika uchumi wa Buluu. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Ununuzi wa meli ya pili ya uvuvi umefanyika na umefikia asilimia 80 ya uundaji na malipo. Uundaji wa meli hio umechelewa kutokana na maradhi

ya COVID 19 nchini Srilanka, hivyo meli hiyo inatarajiwa kukamilika na kufika Zanzibar baada ya kupungua kwa maradhi hayo nchini Srilanka,

ii. Tani 10 za samaki aina ya Jodari, Sehewa, Mbasi na Sansuri wamevuliwa na kuingizwa katika soko la Zanzibar.

iii. Matayarisho ya Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa Fungurefu umefikia hatua zifuatazo:

a) Kukamilika kwa michoro ambayo inasubiri ruhusa ya uthibitisho (approval) kutoka Mamlaka ya Majengo.

b) Kuandaa nyaraka za kibiashara (Bankable Documents) kwa ajili ya matumizi ya Benki na taasisi za kifedha ili kuweza kupata mtaji wa ujenzi wa kiwanda au kuingia makubaliano ya pamoja na Kampuni zitakazokuwa tayari kuwekeza Zanzibar.

c) Kufanya mazungumzo na Mashirika na Taasisi za Kifedha kuhusu uwekezaji katika kiwanda. Aidha, Mashirika hayo yameonesha utayari wa kushirikiana na ZAFICO katika uwekezaji huo na wanasubiri maelekezo ya Serikali.

iv. Matayarisho ya Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata minofu ya Samaki Malindi na miundombinu ya baridi kwa ajili ya kuhifadhia Samaki umefikia hatua zifuatazo:

a) Michoro ya kiwanda imekamilika na kuwasilishwa

UNESCO kupitia Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

b) Kukamilika kwa nyaraka za kibiashara (Bankable Documents).

v. Kufanya mazungumzo na Mashirika na Taasisi za Kifedha kuhusu uwekezaji katika kiwanda. Mashirika hayo yameonesha utayari wa kushirikiana na ZAFICO katika uwekezaji huo na wanasubiri maelekezo ya Serikali.

vi. Maandalizi ya kuanzishwa kwa shamba la ufugaji wa Samaki baharini katika eneo la Mkokotoni yameshaanza kwa kuanzisha Kampuni ya pamoja baina ya ZAFICO na Willing Hands kutoka Norway na Onyx Stone inayowakilisha mfuko wa hifadhi ya jamii ya Oman. Kampuni hiyo imeshasajiliwa na inaitwa "Zanzibar Aquaculture Harvest Company" (ZAHC).

vii. Jumla ya wafanyakazi 5 wamepatiwa Mafunzo kwa ajili ya kukuza uwezo wao kiutendaji kati ya wafanyakazi 10 ambao walitarajiwa kupata mafunzo hayo.

viii. Jumla ya vikundi 8 vya uvuvi vimepata mafunzo jinsi ya kuvua dagaa na samaki wa jodari kwa ajili ya kuchakata na kuuza nje ya nchi.

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) ilipanga kutumia jumla ya TZS 3.69 bilioni (TZS 2.01 bilioni kwa kazi za kawaida pamoja na Mishahara na TZS 1.69 bilioni kwa ajili ya

Miradi ya Maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2021 Kampuni imetumia **TZS 1.429 bilioni (TZS 584 milioni** kwa matumizi ya kawaida na mishahara na **TZS 844 milioni** kwa Miradi ya Maendeleo) sawa na asilimia **39** ya fedha zilizopangwa. **(Kiambatisho Nam 5).**

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**39.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Udhibiti wa Ufuatiliaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia dhumuni lake kubwa ni kuendelea na kazi ya Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kuhakikisha Zanzibar inafaidika na Rasilimali hiyo. Programu hii imegawika katika maeneo mawili ambayo: Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

**40.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Programu ya Udhibiti wa Ufuatiliaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia iliombewa **TZS 5.78 bilioni (TZS 458.92 milioni** ni Ruzuku ya Mishahara, **TZS 1.03 bilioni** kwa ajili ya Ruzuku ya matumizi mengineyo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na **TZS 4.28 bilioni** kwa ajili ya Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (**TZS 712 milioni** mishahara, **TZS 3.57 bilioni** kwa kazi za kawaida). Hadi kufikia Machi, 2021 Programu imepata **TZS 1.74 bilioni** (**TZS 421.16 milioni** mishahara, **TZS 319.11 milioni** kwa kazi za kawaida kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na

Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na **TZS 1.0 bilioni** kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia) sawa na asilimia **30** na asilimia **37** kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

## Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA)

**41.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ni taasisi yenye jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar. Aidha, kwa mwaka 2020/2021 Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Rasimu tano (5) za Kanuni na Miongozo ya Kitaalamu kwa ajili ya kusimamia shughuli za Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar zimetayarishwa. Rasimu hizo ni: -

a) Rasimu ya Kanuni ya Mgawanyo wa Vitalu (Graticulation Regulation).
b) Rasimu ya Kanuni ya Utoaji wa Zabuni (Tendering Regulation).
c) Rasimu ya Kanuni ya Thamani ya Wadau wa Ndani (Local Content Regulation).
d) Rasimu ya Kanuni ya Wafanyakazi wa Mamlaka (Staff Regulation).
e) Rasimu ya Kanuni ya Utafiti wa Awali, Mitetemo

na Uwasilishaji wa taarifa za Utafiti kwa Mamlaka (Reconnaissance, Seismic and Data submission Regulation).

ii. Programu 64 za kujenga uelewa kwa wananchi zimeendeshwa kati ya Programu 80 zilizopangwa. Programu hizo zilifanyika kwa njia za mikutano, vikao, Televisheni na Magazeti.

iii. Mamlaka imesimamia zoezi la Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya mtetemo (3D Seismic Survey) katika kitalu cha Pemba – Zanzibar. Tayari matayarisho ya kazi ya Uchukuaji wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya Mtetemo wa kina (3D Seismic Survey) yamefanyika kwa lengo la kupata Taarifa za kina za kijiolojia katika eneo la kitalu cha Pemba – Zanzibar.

iv. Mamlaka imetekeleza kazi ya kuhakiki madai ya fidia kwa wananchi walioathiriwa mali zao wakati wa zoezi la mtetemo kwa Kitalu cha Pemba – Zanzibar. Kamati maalum ya fidia (Damage Committee) imeundwa na inaendelea kupitia ripoti ya uhakiki wa idadi ya waathirika na viwango vinavyohitajika kulipwa ili kuweza kuidhinisha hatua za malipo.

v. Timu ya Ukaguzi wa Mkataba wa Mgawanyo wa Mapato (PSA Audit) kwa kazi za kitalu cha Pemba – Zanzibar imeundwa na Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi za TRA, ZEMA, OCAG na

DOSH. Tayari Timu hiyo imeshapatiwa mafunzo maalum kwa ajili ya kazi husika na kwamba kazi hiyo imepangwa kuanza mnamo mwezi wa Juni na kukamilika mwezi wa Agosti 2021.

vi. Mamlaka imekamilisha matayarisho ya zoezi la Utafiti wa Pamoja wa Mafuta na Gesi Asilia (Multi – Client) katika Maeneo ya kina kirefu cha Bahari ya Zanzibar yanayojumuisha Mapitio ya Modeli ya Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2017 (Model of Production Sharing Agreement – MPSA), Kuandaa Rasimu ya Mkataba wa Uchukuaji wa Taarifa za Mtetemo (The Draft Agreement for Multi – Client 2D Sesismic Data Acquisition, Processing, Interpretation, Marketing and Licensing for the Offshore Area) na kuandaa Rasimu ya Utangazaji wa Zabuni ya Uchukuaji wa Taarifa za Mtetemo (Request for Proposal - RFP).

vii. Kuimarishwa mfumo wa usimamizi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia kwa kujenga chumba cha muda cha kuhifadhia Taarifa (Temporary data center) pamoja na kushiriki mafunzo ya vitendo kwa wataalamu wake huko Dar es Salaam katika ofisi za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania – TPDC.

viii. Jumla ya semina tano (5) za mashirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi zimeendeshwa kwa ajili ya Maendeleo ya Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

ix. Jumla ya wafanyakazi watatu (3) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Shahada ya Pili na jumla ya mafunzo 54 ya muda mfupi yametolewa kwa wafanyakazi wa Mamlaka kwa ajili ya kuleta ufanisi zaidi kwa watendaji.

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia iliombewa **TZS 1.3 Bilioni** kwa kazi za kawaida, **TZS 458.92** ni Ruzuku ya Mishahara. Hadi machi 2021, Mamlaka imepatiwa jumla ya **TZS 740.27 milioni** sawa na asilimia **57** ya fedha zilizoombwa na asilimia **66** kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

## Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (ZPDC)

42. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia ina jukumu kubwa la kushiriki katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kufanya biashara katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa niaba ya Serikali na kulinda maslahi ya Taifa katika biashara ya Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kampuni ilipanga kutayarisha Kanuni 3 ambazo ni Kanuni za Wafanyakazi (Staff Regulations), Kanuni za uendeshaji wa shughuli za kifedha (Financial Regulations) na Muongozo wa

uendeshaji wa shughuli za Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni (Board Charter) ambapo Kanuni na Miongozo hiyo imetayarishwa na kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni.

ii. Kampuni katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 iliunganisha huduma ya intaneti, miundombinu ya Tehama (Network), mfumo wa Kamera za ulinzi (CCTV), mfumo wa mawasiliano ya ndani (IP phone), mfumo wa mahudhurio ya Wafanyakazi kazini (Biometric attendance), kufanya matengenezo ya ofisi, ununuzi wa samani za ofisi pamoja na ununuzi wa gari.

iii. Kampuni ilifanya ziara za kimafunzo za ndani ya nchi katika Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC), Kampuni tanzu za TPDC ya GASCO ya uchakataji wa Gesi Asilia na TANOIL ya ununuzi na uuzaji wa Mafuta, Bohari ya Mafuta TIPER na Wakala wa Uagiziaji wa Mafuta kwa pamoja Tanzania (TPBPA).

iv. Jumla ya mafunzo 13 ya ndani ya nchi kati ya mafunzo 16 yanayohusiana na Mafuta na Gesi Asilia yalitolewa na Kampuni ikiwa ni sawa na asilimia 81 ya shabaha iliyowekwa.

v. Jumla ya mafunzo 8 ya ndani ya nchi kati ya mafunzo 10 yaliyopangwa yametolewa na

Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia sawa na asilimia 80.

vi. Kampuni imefanya vikao 10 na mkandarasi RAK Gas vya usimamizi wa leseni kati ya vikao 12 vilivyopangwa sawa na asilimia 83 ya shabaha.

vii. Kampuni imefanya programu 7 za kutoa uelewa katika Mafuta na Gesi Asilia kwa Wadau. Miongoni mwa wadau waliopata uelewa huo ni pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya SMZ (CAG), Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA), Shirika la Bandari (ZPC), Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia ilitenga **TZS 4.28 bilioni** kwa kazi za kawaida. Hadi Machi 2021, Kampuni imetumia jumla ya **TZS 1.10 bilioni** (Mishahara **TZS 372 milioni** na Kazi za Uendeshaji **TZS 729.89 milioni)** sawa na asilimia **26** ya fedha zilizoombwa na asilimia **31** kwa fedha zilizopangwa miezi tisa. (Kampuni ilikua na bakaa la mtaji la **TZS 1.6 bilioni** kuanzia mwezi wa Machi 2020).

## PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA WIZARA

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara, Programu ndogo ya Uendeshaji na Utawala na Programu Ndogo ya Utawala na Ofisi Kuu Pemba.

45. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi kifupi cha kuundwa kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya nane, programu imeweza kutekeleza mambo machache ya msingi. Aidha, kwa kiasi kikubwa na kabla ya kuundwa kwa Wizara hii mpya kazi za uratibu zilifanywa kupitia wizara nyengine za awali.

46. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Mipango, Utawala na usimamizi wa kazi za Wizara iliombewa jumla ya **TZS 1.41 bilioni** (**TZS 1.27 bilioni** mishahara, **TZS 138.3 milioni** kazi za kawaida,). Hadi kufikia Machi, 2021 Programu imepata jumla ya **TZS 158.0 milioni** (**TZS 119.09 milioni** mishahara, **TZS 38.9 milioni** kazi za kawaida sawa na asilimia **13** ya fedha zilizoombwa na asilimia **15** kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

## Programamu ndogo ya Mipango na usimamizi wa Kazi za Wizara

47. **Mheshimiwa Spika,** Dhumuni la programu hii ni kusimamia na kuratibu, Sera, Sheria, Mikakati na Mipango ya maendeleo na Utafiti, pamoja na kuratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi zikiwemo washirika wa maendeleo na sekta binafsi. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Ufuatiliaji na tathmini wa kazi za Wizara na Miradi mitatu ya maendeleo ikiwemo mradi wa Ujenzi wa diko na soko la samaki Malindi, Mradi wa usimamizi wa Bahari Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOfish) na Mradi wa kutotoa vifaranga vya samaki (Hatchery) umefanyika.

ii. Mikutano sita ya mashirikiano imefanyika ikiwemo:

- Mkutano baina ya Wizara ya Uchumi wa Buluu SMZ na Wizara ya Mifugo na Uvuvi SMT imefanyika na kujadili suala la Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu na utekelezaji wa Miradi ya pamoja.
- Kufanyika kwa ziara za pamoja za ukaguzi wa miradi baina ya Wizara ya Uchumi wa Buluu SMZ na Wizara ya Nchi Afisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Mkutano wa kusaini Kanuni za Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, 2021 ulioshirikisha Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi SMZ na Wizara ya Mifugo na Uvuvi SMT
- Mkutano wa kusaini mkataba wa ongezeko la muda na upatikanaji wa fedha za ziada wa mradi wa Soko la Malindi umesainiwa baina ya Shirika la Maendeleo Japani na Afisi ya Rais (Fedha na Mipango) Zanzibar.
- Kuwezesha kusainiwa kwa Mikataba ya mjenzi (Nissan and RINKAI Company Limited - Japan) na mshauri muelekezi (Fisheries Engineering Company - Japan) wa Soko la Malindi (LOT 1 na LOT 2).
- Kuwasilishwa na Kuorodheshwa katika Baraza la Wawakilishi kwa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020.

iii. Kukamilisha matayarisho yaliyopelekea kuanza kwa mradi mpya wa Uvuvi Zanzibar chini ya ufadhili wa IFAD kwa thamani ya **U$D 8.8 Milioni** sawa na **TZS 20.2 Bilioni**.

iv. Sera ya Uchumi wa Buluu Zanzibar imeshaanza kufanyiwa mapitio ikiwemo Rasimu ya awali ya Mpango Mkakati wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi ambayo imo katika hatua nzuri za matayarisho.

v. Kusainiwa kwa hati ya makubaliano baina ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Kampuni ya INTERTORCO. Aidha, jumla ya miradi kumi inategemewa kutekelezwa baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu (Feasibility Study) ya programu ya Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Mpigaduri na Mkoani Pemba.
vi. Kuratibu ziara na vikao viwili (2) vya kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

48. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 programu ndogo ya Mipango na Usimamizi wa kazi za Wizara imeombewa jumla ya **TZS 74.3 milioni** (**TZS 43.8 milioni** mishahara na **TZS 30.5 milioni** kazi za kawaida). Hadi kufikia Machi 2021 programu ndogo hii imetumia jumla ya **TZS 12.9 milioni** (**TZS 6.91 milioni** kwa mishahara na **TZS 6 milioni** kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia **17** ya fedha zilizoombewa na asilimia **32** kwa fedha zilizopangwa kwa miezi mitatu ya utekelezaji wa Wizara.

## Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

49. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Madhumuni ya programu hii ni kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu.

Aidha, programu inaratibu masuala ya haki na wajibu wa wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria na kanuni za utumishi Serikalini pamoja na kuratibu masuala mtambuka ikiwemo Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kukamilisha ukaguzi wa ndani wa mahesabu ya miradi 3 na Kampuni ya Mendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia umefanyika
ii. Kukamilisha vipindi (new story) 3 vya redio na televisheni vyenye kuhamasisha Uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini vimetayarishwa.
iii. Jumla ya **TZS 3,423,438** zimelipwa kwa wafanyakazi 21 ikiwa ni fedha za likizo **TZS 1,200,000** na malipo ya muda wa ziada **TZS 2,223,438.**
iv. Matayarisho ya muundo wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na Idara mpya zilizoelekezwa imekamilika na kuwasilishwa Kamisheni ya Utumishi Serikalini. Aidha mahitaji ya wafanyakazi wa taasisi mpya ya Wizara Uchumi wa Buluu na Uvuvi yamewasilishwa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

**50.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Programu ndogo ya Utawala na Mafunzo,

iliombewa jumla ya **TZS 571.19 milioni** kwa kazi za kawaida (**TZS 488.4 milioni** ni mishahara na **TZS 82.7 milioni** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2021 Programu imepatiwa **TZS 74.82 milioni** (**TZS 54.8 milioni** kwa mishahara na **TZS 20 milioni** kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia **13** na asilimia **27** kwa fedha zilizopangwa kwa miezi mitatu ya utekelezaji wa Wizara hii.

## Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba

**51. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ofisi Pemba imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu na kufanikisha vikao 2 na ziara za Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini na vituoni;
iii. Vikao 4 vya uendeshaji na usimamizi wa ofisi kuu Pemba vimefanyika kwa kushirikiana idara na taasisi mbali mbali mtambuka za sekta ya Uchumi wa Buluu na uvuvi - Pemba;
iv. Uratibu wa ziara za wageni na viongozi wa Wizara

umefanyika kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Wizara

v. Mashirikiano na taasisi nyenginezo (Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii) yameimarishwa.

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, iliombewa **TZS 770.68 milioni (TZS 745.6 milioni** mishahara na **TZS 25 milioni** ni matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2021 programu imepata **TZS 70.27 milioni** (**TZS 57.35 milioni** mishahara na **TZS 12.91 milioni** kazi za kawaida) sawa na asilimia **9** na asilimia **22** kwa fedha zilizopangwa kwa miezi mitatu ya utekelezaji wa Wizara hii.

## CHANGAMOTO

53. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada za Wizara na Serikali kwa ujumla, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa ni pamoja na:

i. Kujitokeza kwa Uvuvi haramu na baadhi ya wavuvi kutofuata taratibu za Uvuvi endelevu pamoja na wizi wa mazao ya baharini;
ii. Mabadiliko ya tabia nchi yanayopelekea athari za kimazingira na kusababisha majanga asilia yanayohusiana na bahari na fukwe;
iii. Uwekezaji mdogo katika Sekta ya uvuvi;
iv. Masharti magumu ya mikopo ya benki kwa wavuvi

na wajasiriamali wa Sekta ya Uchumi wa Buluu (Sustainable Blue Economy Financing);

v. Mchakato mrefu wa uthibitishwaji wa Miundo ya Utumishi kwa Taasisi za ZPRA, ZPDC, ZAFIRI, ZAFICO na DSFA;
vi. Uhaba wa teknolojia, nyenzo na wataalamu wa kufanya tafiti bora za uvuvi na mazao ya baharini zitakazosaidia malengo ya utekelezaji wa Sera na mipango ya Uchumi wa Buluu;
vii. Uwepo wa Gharama kubwa za uendeshaji katika masuala ya utafiti na doria;
viii. Kuathirika kwa mnyororo wa thamani (Value chain) wa Sekta ya Uvuvi kutokana na janga la COVID 19;
ix. Changamoto katika utekelezaji wa shughuli za Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia hasa katika utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watendaji wa Kampuni kutokana na kuwepo kwa janga la COVID 19.

**HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

i. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi husika zinaendelea kutoa elimu na kuimarisha doria ili kupunguza uvuvi haramu na uchafuzi wa mazingira ya bahari;
ii. Kuendelea kutoa elimu kwa wakulima wa mwani kulima katika maji ya kina kirefu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

iii. Wizara imeingia katika mikataba ya awali ya ubia (Feasibility Study) na kampuni ya Intertorco (Ujenzi wa Bandari za Uvuvi Mpiga Duri na Mkoani) pamoja na AGTEK Tanzania Limited (Uimarishaji wa uzalishaji, usambazaji na uvunaji wa vifaranga vya Samaki, majongoo bahari, kaa, n.k) katika Sekta ya uvuvi;
iv. Mikataba mingine ambayo tayari imepatiwa ushauri wa kisheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni pamoja na Mkataba wa Onyx/ Willing Hands ya Uvuvi wa Matenga (Fish Cage Farming), pamoja na ile ya ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa Fungu Refu – Mkokotoni; na Minofu ya Samaki – Malindi chini ya mashirikiano ya ubia na kampuni ya CANITAN;
v. Kuorodhesha Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020 na utekelezaji wa Kanuni ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, 2021;
vi. Kufanya mazungumzo na Taasisi za Fedha za ndani na nje kwa ajili ya kutoa fursa ya mikopo yenye masharti nafuu katika utekelezaji wa mipango na mikakati ya Uchumi wa Buluu;
vii. Kuendelea kufuatilia hatua zilizofikiwa katika kuidhinishwa miundo ya Taasisi;
viii. Kutoa mafunzo kwa mabaharia, wasarifu wa dagaa na wakuu wa madiko juu ya mbinu za uvuvi wa kitaalamu na kuongeza thamani ya bidhaa zao;

ix. Kununua mtego wenye teknolojia bora na kuongeza idadi ya ndoana kwa lengo la kuongeza kiwango cha uvunaji wa samaki na:
x. Kuongeza boti ili kupunguza gharama za mahitaji ya safari za uvuvi pamoja na uendeshaji;

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**54.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 2.259 bilioni** kutoka vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba **(Kiambatanisho Nam. 6).**

## MAKADIRIO YA MATUMIZI 2021/2022

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 itatekeleza malengo yake kupitia Programu zake kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;
ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi;
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara itatekeleza jumla ya Miradi sita ya Maendeleo kama ifuatavyo:

i. Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi – Southwest Indian Ocean Fisheries (SWIOFish).

ii. Mradi wa Ujenzi wa Diko na Soko la Malindi.
iii. Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (IFAD) Halikadhalika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ipo katika hatua za awali za hati za mashirikiano na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ifuatavyo:
iv. Mradi wa Kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki na vyumba vya baridi
v. Mradi wa Uvuvi wa Matenga katika Bahari ya Kisiwa cha Popo
vi. Mradi wa Kiwanda cha kusarifu dagaa, Fungurefu – Mkokotoni

Pia kwa mashirikiano ya Sekta Binafsi chini ya mfumo wa PPP Wizara imeanza mazungumzo ya awali pamoja na upembuzi yakinifu kwa baadhi ya miradi ambayo pia inategemewa kutekeleza mradi wa kutotolea vifaranga vya Samaki, Kaa na Majongoo Bahari (Marine Hatchery). Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa na Sekta binafsi kupitia Kampuni za AGTEK Tanzania Ltd na Shazain Fisheries ambazo kwa sasa zimo katika hatua za awali za hati za mashirikiano na kwa wao kutayarisha Upembuzi yakinifu (Feasibility Study) wa mradi.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kutekeleza programu hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Wizara inaombewa kutumia jumla ya **TZS 58.54 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 5.65 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS 1.681 bilioni** Mishahara na **TZS 2.026 bilioni** matumizi mengineyo na **TZS 1.947 bilioni** RUZUKU kutoka SMZ

(**TZS 299.1 milioni** kwa ajili yaTaasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao Baharini na **TZS 1.648 bilioni** kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia) **(Kiambatanisho Nam. 7).** Kwa kutekeleza programu na Miradi ya Maendeleo.Wizara inaombewa jumla ya **TZS 52.88 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 16.63** bilioni kutoka SMZ na **TZS 36.25 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo **(Kiambatanisho Nam. 8)**. Jumla ya **TZS 3.0 bilioni** zimetengwa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO inatarajia kupata jumla ya **TZS 43.11 bilioni** kutoka vyanzo mbalimbali kwa utekelezaji wa miradi ya kampuni hio.

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inathamini mchango wa Serikali pamoja na kutoa kipaumbele cha pekee katika kuendeleza sekta ya Uchumi wa Buluu nchini.

## MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

58. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kuendeleza na kukuza Uchumi wa Buluu na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imeweka shabaha za utekelezaji kupitia Programu Kuu tatu na

Programu ndogo sita na huduma zifuatazo:

**PL0201 Maendeleo ya Uchumi wa Buluu**

**SL020101 Maendeleo ya Uchumi wa Buluu**

- Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla
- Uthibiti na uendelezaji wa mafuta na Gesi Asilia

**PL0202 Maendeleo ya Uvuvi**

**SL020201 Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya baharini**

- Kuendeleza Uvuvi wa kienyeji, ukulima wa mwani kwa kutumia teknologia bora na kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini

**SL020202 Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari**

- Kuendeleza uhifadhi wa rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu

**PL0203 Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi**

**SL020301 Utawala na Uendeshaji**

- Utoaji maslahi kwa wafanyakazi na uwekaji wa mazingira bora ya kazi
- Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi
- Kusimamia na kudhibiti mali za Serikali

**SL020302** Mipango, Sera na Tafiti

- Uandaaji na Usimamizi wa Sera, Sheria na Mikakati ya Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi
- Uimarishaji na utoaji wa taarifa za Takwimu za Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi
- Uendelezaji wa Tafiti za kiuchumi na kijamii za sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

**SL020303** Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu - Pemba

- Kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

## MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA 2021/2022.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane imeunda Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa lengo la kubadilisha muelekeo wa Uchumi wa Zanzibar kwa:

i. Kuijenga Zanzibar mpya yenye Uchumi wa Kisasa kwa kuzingatia matumizi endelevu ya Bahari na ukanda wa Pwani.
ii. Kusimamia, kuratibu na kuimarisha maendeleo ya Uchumi wa Buluu Zanzibar ikiwemo Uvuvi na utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia.
iii. Kuimarisha mazingira mazuri ya mashirikiano, uwekezaji na utekelezaji pamoja na sekta binafsi katika sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

iv. Kuimarisha nguvu za uzalishaji, miundombinu, ubora wa mazao ya baharini, na utafutaji wa masoko katika sekta ya uvuvi, mwani na mazao ya baharini hususan katika uwezeshaji wa jamii ndani ya sekta hizi.
v. Kuendeleza uhifadhi bora, endelevu na imara wa maeneo ya bahari kwa kushirikisha jamii, kuinua mapato, na kuhifadhi mazingira.
vi. Kuimarisha na kujenga uwezo wa matumizi ya teknolojia katika doria na uhifadhi wa maeneo ya bahari ili kupunguza gharama za uendeshaji.
vii. Kuimarisha tafiti zinazohusiana na sekta mbali mbali za Uchumi wa Buluu na kuongeza ubunifu, matumizi ya teknolojia ya kisasa, na mipango kazi itakayosaidia utekelezaji wa Sera na Mikakati yetu ya Uchumi wa Buluu.
viii. Kuongeza nguvu katika utekelezaji wa mipango ya uwekezaji, ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya uchumi wa buluu ikiwemo utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia; ujenzi wa bandari mpya za uvuvi; uimarishaji wa uvuvi wa bahari kuu, ujenzi wa mitambo na viwanda vya kuhifadhi, kusarifu na kuchakata Dagaa na Samaki, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya uvuvi wa matenga (Fish Cage Farming).
ix. Uwezeshaji wa jamii katika sekta ya uvuvi mdogo mdogo, na ufugaji wa mazao ya baharini kama samaki, kaa, pweza na majongoo bahari, ukulima wa mwani, na katika kuunga mkono juhudi za

wanajamii za kuingia katika uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya baharini na mwani.

x. Kwa kushirikiana na taasisi husika, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi itatekeleza miradi ya kiuchumi kwa kuzingatia sheria za ndani na mikataba ya kimataifa kuhusu Ulinzi na Usalama Baharini (Maritime Safety and Security).

xi. Kwa kushirikiana na Taasisi husika, Wizara yangu pia itasimamia kwa karibu zaidi uanzishwaji na ufanyaji kazi wa kiwango kinachokubalika kimataifa wa Taasisi ya viwango (Competent Authority) ili ikidhi haja ya shughuli za uzalishaji na usafirishaji wa rasilimali za bahari. Vilevile, Wizara itatekeleza malengo yafuatayo:

a) Kuendeleza Mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na kuhamasisha uwekezaji;
b) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Uvuvi na Mafuta na Gesi Asilia;
c) Kushajihisha wavuvi kufanya uvuvi katika njia rafiki kutokana na matakwa na viwango vya kibiashara;
d) Kushirikiana na Sekta binafsi kuwapatia wavuvi zana za kisasa za Uvuvi na mikopo ya kuendeleza shughuli za Uvuvi na mazao ya baharini;
e) Kujenga masoko ya samaki ya kisasa na ya kimataifa;
f) Kujenga viwanda vya kuchakata na kusarifu samaki, kusarifu mbolea itokanayo na mabaki ya samaki pamoja na Ujenzi wa vyumba baridi vya

kuhifadhia samaki (Cold Storage facilities);

g) Kuimarisha zao la mwani kwa kuongeza bei, kuwapatia vifaa wakulima, kujenga viwanda vya kusarifu mwani na kutafuta masoko mapya ya zao hilo;

h) Kuanzisha miundombinu ya maabara ya viwango (Accredited Laboratory and Competent Authority) itakayowezesha biashara ya kimataifa ya kusafirisha samaki nje ya mipaka ya Tanzania.

i) Kujenga Viwanda vya kutengeneza meli za uvuvi na viwanda vya kutengeneza zana za uvuvi;

j) Kuanzisha Shamba la Ufugaji wa Samaki kwenye matenga (Cage Farming) baharini;

k) Kushirikiana na Ubalozi wa Indonesia Nchini Tanzania kwa lengo la kutupatia Samaki Mama aina ya Mwatiko pamoja na fursa za wataalamu wa Zanzibar kujifunza njia bora za kutotolea vifaranga vya Samaki;

l) Kuendesha kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki kwa mfumo wa mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP);

m) Kuendelea kushirikiana na Taasisi mbali mbali zenye dhamira ya kuiwezesha nchi katika Sekta ya Uvuvi;

n) Kuifanya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini kuwa kituo bora cha utafiti na ushauri elekezi wa Uvuvi na rasilimali za baharini katika ukanda wa Bahari ya Hindi;

o) Kuendeleza na kukuza tafiti za kisasa kwa kutumia

teknojia za kisasa, na mbinu za kisasa juu uvuvi, rasilimali za bahari, na mifumo na mienendo ya bahari (Oceanographic research);

p) Kuanza utafiti mkubwa wa kutambua rasilimali za Baharini zilizopo katika Bahari ya ndani (Comprehensive marine inventory in Territorial Sea)

q) Kuendelea na hatua za tafiti za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia;

r) Kuziimarisha kwa kuzijengea uwezo wa kitaalamu na nguvu kazi Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA);

s) Kuendelea kushirikiana na Kampuni zenye dhamira ya kuwekeza nchini katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia;

t) Kushiriki katika biashara ya Mafuta na Gesi Asilia katika Mkondo wa Chini;

u) Kuziandaa Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali kuweza kushiriki katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia (local content);

v) Kujenga uelewa kwa jamii na Taasisi mbali mbali juu ya Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia;

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

60. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu imegawika katika programu ndogo moja nayo ni programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Aidha Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ina huduma zake kuu mbili nazo ni:

    i. Uratibu wa Uchumi wa Buluu
    ii. Udhibiti wa Ufuatiliaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

61. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu dhumuni lake kubwa ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla, Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 2.44 bilioni** kwa matumizi ya kawaida (**TZS 799.8 milioni** ni matumizi mengineyo na **TZS 1.648 bilioni** RUZUKU ya kazi za kawaida)

### Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu inalenga kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla.

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu ndogo ya Uchumi wa Buluu kupitia huduma ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu inalenga kutekeleza shabaha

zifuatazo:

i. Ushirikishwaji wa wadau wa sekta katika kufanya mapitio ya Sera ya Uchumi wa Buluu,
ii. Kuanzisha mfuko maalumu wa maendeleo ya Uchumi wa Buluu,
iii. Kuandaa mfumo maalumu (Dash board) kwa ajili ya uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu,
iv. Kuandaa kanuni na miongozo ya kitaalamu kwa sekta za Uchumi wa Buluu,
v. Kuandaa programu na vipindi maalum vya uelewa kwa shughuli zinazoendeshwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na:
vi. Kuendeleza mashirikiano na taasisi za ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa,

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 799.8 milioni** kwa matumizi ya kawaida.

## Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA)

65. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inalenga kuendeleza majukumu yake ya kusisamia na kudhibiti shughuli zote za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

66. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa

Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuandaa rasimu nne (4) za Kanuni za Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia
ii. Kuendesha programu 50 za kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu masuala ya Mafuta na Gesi Asillia.
iii. Kuendelea kusimamia zoezi la utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa kitalu cha Pemba-Zanzibar.
iv. Kusimamia zoezi la utafiti wa pamoja (Multi client) wa Mafuta na Gesi Asilia katika maeneo ya bahari ya mashariki ya Zanzibar ili kuweza kupata taarifa zitazosaidia katika ugawaji wa vitalu na ufunguaji wa maeneo mapya ya uwekezaji.
v. Kuendelea kuimarisha na kusimamia Mfumo wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia, Wadau wa Sekta pamoja na kutoa taarifa na machapisho zinazouhusiana na shughuli za Mafuta na Gesi Asilia.
vi. Kuendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuimarisha taasisi na kuwapatia watendaji nafasi za mafunzo yanayohusiana na usimamizi wa Mafuta na Gesi Asilia.
vii. Kushiriki katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ya kitaifa, kikanda na kimataifa.
viii. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa watendaji ikiwemo ubora wa ofisi, nguvu kazi pamoja na

kuwapatia mafunzo wafanyakazi waliopo ili kuleta ufanisi zaidi kwa Mamlaka.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inaombewa jumla ya **TZS 1.648 bilioni,** kati ya fedha hizo (**TZS 1.096 bilioni** kwa matumizi ya kawaida ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini na **TZS 551.7 milioni** ni Mishahara).

## Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC)

**68.** **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inalenga kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni

**69.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kujenga uwezo kwa Watendaji wa Kampuni katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia;
ii. Uendeshaji wa shughuli za Mkataba wa mgawanyo wa Mafuta na Gesi Asilia (PSA);
iii. Ununuzi wa vifaa vya kuhifadhia taarifa za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwa Majiolojia pamoja na kuanzisha mfumo

wa akiba wa kuhifadhi taarifa za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia;

iv. Kutoa uelewa wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi za Serikali na wananchi.

70. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inaombewa jumla ya **TZS 3.0 bilioni** kwa matumizi ya kawaida na Maendeleo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

71. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni:

i. Programu ndogo ya Maendeleo ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini;
ii. Programu ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari;

72. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 54.321 bilioni**, kati ya hizo **TZS. 1.433 bilioni** kwa matumizi ya kawaida (**TZS 538.19 milioni** ni Mishahara, **TZS 596.32 milioni** ni matumizi mengineyo na **TZS 299.1 milioni** ni Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Mazao ya Baharini (ZAFIRI)) na **TZS 52.888 bilioni** kwa ajili ya

Miradi ya Maendeleo (**TZS 16.63 bilioni** kutoka SMZ na **TZS 36.25 bilioni** kutoka kwa Washirika wa maendeleo).

## Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Bahari;

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na ufugaji wa mazao ya bahari inalenga kuendeleza uvuvi kwa kutumia taknologia bora na kuendeleza ufugaji/ ukulima wa mazao ya baharini.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza kilimo cha mwani na kuongeza uzalishaji kutoka tani 9,000 hadi zaidi ya 12,000 kwa kuwapatia wakulima mafunzo bora ya uzalishaji wa mwani na kuwapa nyenzo zitakazosaidia kufanya usarifu wa mwani.
ii. Kuendeleza mashamba 12 ya mfano ya ufugaji wa mazao ya baharini Unguja (4) na Pemba (8).
iii. Kuwapatia mafunzo ya ufugaji wa mazao ya baharini vikundi 131 Unguja (73) na Pemba (58), pamoja na wanajamii wengine.
iv. Kuwawazesha wavuvi wadogo wadogo 150 (Unguja 75 Pemba 75) kuweza kuvua kwenye maji ya kina kirefu kwa kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na taasisi za mikopo kuweza kupatiwa mikopo.
v. Kukamilisha utayarishaji wa mpango mkuu wa

uvuvi (2019-2033) na Sera ya Uvuvi na kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 7 ya mwaka 2010, na Kanuni Kuu za Uvuvi za mwaka 1993. Pamoja na kukamilisha kanuni kuu za maeneo ya hifadhi za bahari na kuanzisha sheria ndogondogo za usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika vijiji vilivyomo pembezoni mwa bahari.

vi. Kukamilisha ujenzi wa soko la kisasa la samaki la Malindi ikiwemo uwekaji wa mitambo ya barafu na jengo la biashara lenye uwezo kuhudumia watu 6500 kwa wakati mmoja,

vii. Kufanikisha ujenzi wa kituo cha kupokelea vifaranga vya samaki Wilaya ya Mkoani Pemba. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kupokea na kuhifadhi wastani wa vifaranga 20,000 vya samaki, majongoo bahari na kaa kabla ya kuwasambaza kwa wananchi.

viii. Kuendesha kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki kwa mfumo wa mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP).

**75.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu ndogo hii inaombewa **TZS 54.021 bilioni** kati ya hizo **TZS. 1.133 bilioni** kwa kazi za kawaida (**TZS 538.19 milioni** ni mishahara, **TZS 296.32 milioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 299.1 milioni** ni ruzuku kwa ajili ya taasisi ya utafiti wa uvuvi na mazao ya baharini) na **TZS. 52.88 bilioni** kwa kazi za maendeleo (**TZS 16.63 bilioni** kutoka SMZ na **TZS 36.25 bilioni** kutoka kwa Washirika wa maendeleo).

## Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kufanya tafiti 4 kwa mwaka zinazohusiana na uvuvi, mazao ya Baharini na rasilimali za Baharini na kutowa mrejesho katika jamii.
ii. Kuimarisha miundombinu ya taasisi, kuanzisha na kuimarisha maabara moja ya kuthibiti viwango vya samaki, kuanzisha maabara ya tafiti za mifumo na mienendo ya Bahari (Oceanographic laboratory) na kuanzisha Ofisi na kituo kidogo cha Utafiti Pemba.
iii. Kuchapisha vitabu 500 vya Muongozo wa Ufugaji Majongoo Bahari kwa njia ya Kitaalamu na kuvisambaza kwa wadau.
iv. Kuajiri watafiti na wataalam 32 na kuwajengea uwezo wafanyakazi 14 watakaotoa huduma bora katika kutekeleza tafiti za uvuvi na mazao ya baharini.
v. Kuendeleza mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na mazao ya Baharini.
vi. Kuanza utafiti mkubwa wa utambuzi wa rasilimali za Bahari zilizo katika Bahari ya ndani (Comprehensive Marine inventory for Territorial

water) utakaojumuisha utafiti wa Uchumi wa Buluu na Utalii kwa kuangalia Mabaki ya Kihistoria yaliyopo chini ya bahari.

vii. Kuchapisha vitabu 500 vyenye taarifa za utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini zilizofanyika Zanzibar kuanzia mwaka 1999-2020 kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi.

viii. Kununua vifaa vya kisasa vitakavowezesha kufanyika kwa tafiti bora za uvuvi, rasilimali za Baharini, na mienendo na mifumo ya Bahari

ix. Kuanzisha Jarida la Tafiti za Uvuvi, Rasilimali za Baharini, na mienendo na mifumo ya Bahari

x. Kuandaa kitabu cha taarifa za Tafiti kwa Sera za Uchumi wa Buluu na Uvuvi (Policy Briefs for Blue Economy and Fisheries).

xi. Ununuzi wa vifaa vya Tehama, pamoja na vifaa vya kuhifadhia taarifa za tafiti za Uvuvi, mazao ya Baharini, rasilimali za Baharini, na mienendo na mifumo ya Bahari

**77.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inaombewa jumla ya **TZS 299.1 milioni** kwa matumizi ya kawaida ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

## Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari

**78.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i) Kutoa elimu ya Uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo kamati za uvuvi 91 Unguja (62) na Pemba (29) ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari kwa kuanzisha maeneo ya ufungaji wa pweza na samaki wa miambani.

ii) Kuwawezesha jamii kuweka matumbawe bandia na kufanya ufuatiliaji wa matumbawe katika maeneo ya Hifadhi za bahari (MENAI 5 MIMCA 4 na PECCA 6) ili kuongeza uzalishaji wa samaki.

iii) Kukamilisha kanuni kuu za maeneo ya hifadhi za bahari na kuanzisha sheria ndogondogo za usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika vijiji vilivyomo pembezoni mwa bahari.

Kutekeleza mipango ya usimamizi ya hifadhi kwa kuendeleza kilimo cha mwani na kuongeza uzalishaji kutoka tani 9,000 hadi 12,000 kwa kuwapatia wakulima wa mwani mafunzo bora ya uzalishaji wa mwani na kuwapa nyenzo zitakazosaidia kufanya usarifu wa mwani.

iv) Kuimarisha doria/ulinzi shirikishi 336 katika maeneo ya Maji ya Ndani kwa kununua boti 5 za doria ili kudhibiti uvuvi haramu.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu hii ndogo ya Uhifadhi inaombewa **TZS 300 milioni** kwa matumizi mengineyo ya kazi za kawaida.

## Kampuni ya Uvuvi ZAFICO

80. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) kwa Mwaka wa Fedha 2021-2022, inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

    i. Kuvua tani 120 za Samaki na kuuza katika taasisi za Serikali kampuni na hoteli.
    ii. Kushajihisha vikundi 14 vya wavuvi Unguja na Pemba kufanya uvuvi katika njia rafiki kutokana na matakwa na viwango vya kibiashara.
    iii. Kuanza ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa Mkokotoni Fungu Refu.
    iv Kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchakata minofu ya Samaki pamoja na vyumba vya baridi kwa ajili ya kuhifadhia Samaki.
    iv. Kujenga shamba la ufugaji samaki baharini chini ya usimamizi wa kampuni mpya iliyoanzishwa ya "Zanzibar Aquaculture Harvest Company" (ZAHC).
    v. Kuanzisha miradi miwili mipya ikiwemo ufugaji wa samaki aina ya mwatiko kwa ajili ya chambo na mradi wa kuanzisha mitaala ya masomo ili kuweza kutengeza wataalamu watakaofanyakazi katika viwanda na uvuvi wa bahari kuu.

81. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO inatarajia kupata jumla ya **TZS 43.11 bilioni** kutoka vyanzo mbali ambapo **TZS 1.29** bilioni kutoka mashirika yenye hisa (ZSSF, ZSTC, ZIC na

ZPC) na **TZS 785.36 milioni** ikiwa ni pato litakalotokana na uzalishaji wake kwa kipindi hicho. Aidha uwezekezaji wa jumla ya **TZS 13.033 bilioni** kutoka SMZ na TZS **11.327 bilioni** kwa washirika wa maendeleo (**TZS 3.15 bilioni** IFAD na **TZS 8.18 bilioni** kutoka Oman Investment na Willinghand). Aidha, Kampuni ya ZAFICO inategewa kuchukua mkopo wa **TZS 16.7 bilioni** kwa ajili ya ujenzi wa viwanda viwili vya miradi vya usarifu wa dagaa na uchakataji wa samaki.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi kwa ustawi kwa sekta.

**Programu imegawika katika program ndogo tatu nazo ni:**

i. Programu ya Utawala na Uendeshaji
ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti
iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba

**83.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inaombewa jumla ya **TZS 1.773 bilioni** kati ya hizo (**TZS 1.142 bilioni** ni mshahara, **TZS 630.17 milioni** matumizi mengineyo).

## Programu ndogo ya utawala na uendeshaji

84. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

85. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 proramu hii ndogo inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

    i. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi 55 (Likizo kwa wafanyakazi 50 na muda wa ziada kwa wafanyakazi 5) pamoja na kuwajengea mazingira mazuri ya kazi;
    ii. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 16 (mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 6 na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 10)
    iii. Udhibiti na ufuatiliaji wa mali za Serikali ikiwemo uandaaji wa "Asset register" ya Wizara.
    iv. Kuendelea na ukaguzi wa mahesabu ya ndani kwa kila robo mwaka pamoja na vikao vya zabuni kwa ajili ya upatikanaji wa vifaa na huduma.
    v. Kuendelea kutoa taarifa za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia vyombo vya habari, majarida kwa njia ya mtandao.

86. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, inaombewa jumla ya **TZS 825.31 milioni** kwa kazi za kawaida (**TZS 601.43 milioni** ni mishahara na **TZS 223.88 milioni** kwa matumizi mengineyo).

## Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

87. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

    i. Kuandaa, kupitia Sera, Kanuni na Mikakati ikiwemo Sera ya Uvuvi na marekebisho ya Sheria na Kanuni za Uvuvi.
    ii. Kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Agenda ya Utafiti Zanzibar na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo.
    iii. Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ukusanyaji na usambazaji wa takwimu.
    iv. Kuendeleza mashirikiano na taasisi za ndani, kikanda na kimataifa.
    v. Kuandaa miradi mipya ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na kuratibu usimamizi wa miradi inayoendelea ya Wizara (**Kiambatisho Nam 9A-G**).
    vi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti na mpangokazi wa Wizara ya uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na kuwasilisha utekelezaji kwa mujibu wa

miongozo ya Baraza la Wawakilishi na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

vii. Kuratibu kazi za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya uchumi wa Buluu na Uvuvi.

89. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango inaombewa jumla ya **TZS 250.23 milioni** kati ya hizo **TZS 83.9 milioni** mishahara, **TZS 166.3 milioni** kwa matumizi mengineyo).

## Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara -Pemba

90. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu vikao 4 na ziara za Kamati ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara Pemba.

ii. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, na taasisi zinazosimamiwa na wizara ya Uchumi wa buluu na uvuvi-Pemba.

iii. Kufanya vikao vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana na idara

na taasisi mbali mbali mtambuka za Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Pemba.

iv. Kuratibu ziara za watendaji wa wizara Pemba kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za wizara Unguja na maeneo mengine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

v. Kuratibu ziara za wageni na viongozi wa Wizara kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Wizara pamoja na kuhudhuria katika sherehe na kumbu kumbu za kitaifa Pemba.

vi. Kuimarisha mashirikiano na taasisi nyenginezo za Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii.

vii. Kuongeza mwamko kwa wadau juu ya sera, kanuni na mipango ya uchumi wa buluu na uvuvi-Pemba.

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu hii inaombewa kutumia jumla ya **TZS 697.5 milioni** (**TZS 457.5 milioni** mishahara na **TZS 240.0 milioni** ni matumizi mengineyo).

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 2.259 bilioni** kupitia vianzio vyake vinne vya Unguja na Pemba.

**94. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 58.542 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 5.654 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS 1.681 bilioni** Mishahara na **TZS 2.026 bilioni** matumizi mengineyo na **TZS 1.947 bilioni** RUZUKU kutoka SMZ kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia. Kwa kutekeleza programu na Miradi ya Maendeleo Wizara imetengewa **TZS 52.888 bilioni** (**TZS 16.63 bilion**i kutoka SMZ na **TZS 36.254 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo).

## HITIMISHO

**95. Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa nachukua nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za Uvuvi na Mafuta na Gesi Asilia zikiwemo Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Biashara Maendeleo ya Viwanda; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Ujenzi Mawasilianao na Usafirishaji; Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ; Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto; Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale; Afisi ya Rais, Fedha na Mipango; Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT); Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (SMT) na Wizara

ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya Jamhuri ya Muungano Tanzania.

96. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatoa shukrani pia kwa Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS); Jumuiya ya WIOMSA; Jumuiya ya Mwambao; Uongozi Institute; TNC na WCS. Vilevile, nachukua fursa hii kwa kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza Uvuvi, Mafuta na Gesi Asilia, zikiwemo Japan, China, Korea Kusini, Marekani, Oman na Norway kwa kushirikiana na Wizara katika kuendeleza Sekta ya Uvuvi, Mafuta na Gesi Asilia nchini. Aidha, nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, IFAD, NORAD, UNDP, UNEP, FAO, JICA, UNICEF, KOICA, Jumuiya ya Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi (IORA), Indian Ocean Commission, Kamisheni ya Jodari ya Bahari ya Hindi (IOTC) na Umoja wa nchi za Ulaya (EU).

97. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani za pekee kwa wavuvi na wanakamati za hifadhi za uvuvi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza na kuimarisha uvuvi pamoja na uhifadhi wa rasilimali na ufugaji wa mazao ya baharini. Pia, napenda kumshukuru Katibu Mkuu na Afisa Mdhamini Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi za Wizara yangu pamoja na watumishi wote wa Wizara pasi na kuzisahau Manispaa, Mabaraza ya Mji na Halmashauri na wadau wote wa Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa

Shabaha za Wizara kwa mwaka 2020/2021. Matarajio yetu kwamba tutaendelea kushirikiana tena katika mwaka 2021/2022.


**98.** **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Ulinzi na Usalama, Baraza la Biashara la Taifa, Majukwaa ya Vijana na Kamati za Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya Habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu.

**99.** **Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa** Wajumbe nakushukuruni kwa kunisikiliza na Naomba kuwasilisha.


**MHE. ABDULLA HUSSEIN KOMBO (MBM)**
**WAZIRI, WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ZANZIBAR**

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho Nam. 1a: Uzalishaji wa Samaki (Tani)**



**Kiambatanisho Nam. 1b: Usafirishaji wa Mazao Baharini (Tani)**



## Kiambatanisho Nam. 2: Jadweli la Upatikanaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/21

| Kasma | Maelezo | Makadirio ya Mapato 2020/21 | Mapato halisi Julai hadi Marchi 2021 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | | | | |
| | Leseni Za Uvuvi | 30,000,000.00 | 11,237,500.00 | 37 |
| | Ada Mazao Baharini | 20,000,000.00 | 23,735,450.00 | 119 |
| | Tiketi za Wageni na Faini ( PECCA) | 40,000,000.00 | 3,451,000.00 | 9 |
| **Jumla Ndogo** | | **90,000,000.00** | **38,423,950.00** | 43 |
| **Idara ya Uvuvi** | | | | |
| | Leseni Za Uvuvi | 150,000,000.00 | 29,269,000.00 | 20 |
| | Ada Mazao Baharini | 320,000,000.00 | 219,519,310.00 | 69 |
| | Tiketi za wageni faini na dago (MENAI) | 190,000,000.00 | 149,981,960.00 | 79 |
| | Tiketi za Wageni na Faini (MIMCA ) | 160,000,000.00 | 48,617,841.00 | 30 |
| **Jumla Ndogo** | | **820,000,000.00** | **447,388,111.00** | 55 |
| | | | | |
| Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu | Mapato Ya Uvuvi Wa Bahari Kuu | 1,358,907,360 .00 | 61,394,538.94 | 5 |
| Jumla Ndogo | | 1,358,907,360.00 | 61,394,538.94 | 5 |
| **JUMLA KUU** | | **2,268,907,360.00** | **547,206,599.94** | 24 |

## Kiambatanisho Nam. 3: Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2020- Machi 2021

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | Fedha Iliyopatikana Kwa Kipindi Cha Julai-Machi 2020 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mshahara** | **Matumizi ya Kawaida** | **Ruzuku Kawaida** | **Ruzuku Mishahara** | **Maendeleo SMZ** | **Maendeleo Mhisani** | **Jumla** |
| Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | - | - | 319,110,818 | 421,169,010 | - | - | **740,279,828** |
| MAMLAKA ZPRA | - | - | 319,110,818 | 421,169,010 | - | - | 740,279,828 |
| **PL0104** Maendeleo ya Uvuvi | 590,347,455 | 52,269,646 | 46,345,600 | - | - | 3,149,549,421 | **3,838,512,122** |
| **SL010401** Kuimarisha Ufugaji wa mazao baharini | - | 25,585,138 | - | - | - | - | 25,585,138 |
| **SL010402** Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi ya Bahari | 590,347,455 | 26,684,508 | - | - | - | 3,149,549,421 | 3,766,581,384 |
| SL010402 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari | - | - | 46,345,600 | - | - | - | 46,345,600 |
| **PL0105** Mipango na Usimamizi wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 119,093,585 | 38,912,791 | - | - | - | - | **158,006,376** |
| **SL010501** Utawala na Uendeshaji wa kazi za Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 54,823,285 | 20,000,000 | - | - | - | - | 74,823,285 |
| **SL010502** Mipango, Sera na Ufatifi wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 6,912,750 | 6,000,000 | - | - | - | - | 12,912,750 |
| **SL010502** Uratibu Ofisi Kuu Pemba | 57,357,550 | 12,912,791 | - | - | - | - | 70,270,341 |
| **Jumla Kuu** | **709,441,040** | **91,182,437** | **365,456,418** | **421,169,010** | **-** | **3,149,549,421** | **4,736,798,326** |

**Kiambatanisho Nam. 4: Jadweli la Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo Julai 2020 hadi Machi 2021**

| MRADI | MAKISIO 2020/2021 | | | FEDHA ZILOPATIKANA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | SMZ | MUHISANI | JUMLA | SMZ | MUHISANI | JUMLA |
| Mradi wa usimamizi wa shughuli za uvuvi wa kanda ya kusini mashariki mwa bahari ya hindi **(swiofish)** | | 14,360,003,707.00 | 14,360,003,707.00 | - | 3,149,549,421 | 3,149,549,421 |
| Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindi | 3,475,510,000 | 21,239,604,600 | 24,715,114,600 | - | - | - |
| **Jumla** | **3,475,510,000** | **35,599,608,307** | **39,075,118,307.00** | **-** | **3,149,549,421** | **3,149,549,421** |

**Kiambatanisho Nam. 5: Mchanganuo wa Makadirio na Matumizi kwa Kipindi cha Julai – Machi 2021 (ZAFICO)**

| | Maelezo | Makadirio | Matumizi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mishahara | 594,748,150 | 236,320,500 | 40 |
| 2, | Matumizi ya Kawaida | 1,410,808,240 | 348,100,881 | 25 |
| 3. | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | 1,685,750,000 | 844,776,144 | 50 |
| | **Jumla** | **3,691,306,390** | **1,429,197,525** | **39** |

## Kiambatanisho Nam. 6: Jadweli la Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka 2021/ 2022

| KASMA | MAELEZO | MAKADIRIO YA MAPATO 2021/22 |
|---|---|---|
| **AFISI KUU PEMBA** | | |
| | Leseni za Uvuvi na Chombo anachovulia | 59,066,726 |
| | Ada Mazao Baharini | 44,300,044 |
| | Tiketi za Wageni na Faini ( PECCA) | 81,216,748 |
| Jumla Ndogo | | 184,583,517 |
| **IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI** | | |
| Jumla Ndogo | Leseni ya Uvuvi na Chombo anachovulia | 236.266,902 |
| | Ada ya Usafirishaji wa Mazao ya Baharini | 487,300,486 |
| | Tiketi za Wageni Faini na Dago ( Menai ) | 287,950,287 |
| | Tiketi za Wageni na Faini ( Mimca ) | 239,220,239 |
| | | **1,250,737,914** |
| **MAMLAKA UVUVI WA BAHARI KUU** | | |
| | Uvuvi wa bahari kuu | 1,289,890 |
| **JUMLA KUU** | | **2,259,412,000** |

## Kiambatanisho Nam. 7: Jadweli la Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Kazi za Kawaida kwa Mwaka 2021/2022

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | MAKADIRIO YA FEDHA ZA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2021/2022 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MSHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU KAWAIDA | RUZUKU MISHAHARA | MAENDELEO SMZ | MAENDELEO MHISANI | JUMLA |
| **PL0201** Maendeleo ya uchumi wa buluu | | 800,000,000 | 1,096,500,000 | 551,700,000 | - | - | 2,448,200,000 |
| **SL020101** Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | - | 800,000,000 | - | - | - | - | 800,000,000 |
| Uratibu wa Uchumi wa Buluu | - | 800,000,000 | - | - | - | - | 800,000,000 |
| Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia(ZPRA) | - | - | 1,096,500,000 | 551,700,000 | - | - | 1,648,200,000 |
| **PL0202** Maendeleo ya Uvuvi | 776,995,612 | 600,000,000 | 299,100,000 | - | 16,633,600,000 | 36,254,691,000 | 54,564,386,612 |
| **SL020201** Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya Bahari | 776,995,612 | 300,000,000 | - | - | 16,633,600,000 | 36,254,691,000 | 53,965,286,612 |
| **SL020202** Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari | | 300,000,000 | | | | | 300,000,000 |
| Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari | | | 299,100,000 | | | | 299,100,000 |
| **PLO203** Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 904,104,388 | 626,300,000 | - | - | - | - | 1,530,404,388 |
| **SL020301** Utawala na Uendeshaji | 362,636,765 | 300,000,000 | - | - | - | - | 662,636,765 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **SL020302** Mipango Sera na Utafiti | 83,932,934 | 226,300,000 | - | - | - | - | 310,232,934 |
| **SL020303** Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba | 457,534,688 | 100,000,000 | | | | | 557,534,688 |
| **Jumla Kuu** | **1,681,100,000** | **2,026,300,000** | **1,395,600,000** | **551,700,000** | **16,633,600,000** | **36,254,691,000** | **58,542,991,000** |

## Kiambatanisho Nam. 8: Jadweli la Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka 2021/2022

| MRADI | MAKISIO 2021/2022 | | |
|---|---|---|---|
| | SMZ - TZS | MUHISANI – TZS | JUMLA - TZS |
| Kuanzisha mashamba ya samaki | 463,800,000 | - | 463,800,000 |
| Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Bahari Kuu – SWIOFish | - | 4,606,635,000 | 4,606,635,000 |
| Ujenzi wa Diko na Soko la Malindi | 3,600,000,000 | 21,141,600,000 | 24,741,600,000 |
| Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi | - | 10,506,456,000 | 10,506,456,000 |
| Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa | 4,277,607,000 | - | 4,277,607,000 |
| Ujenzi wa Kituo cha Usarifu na Uhifadhi wa Bidhaa za Samaki | 8,292,193,000 | - | 8,292,193,000 |
| **JUMLA** | **16,633,600,000** | **36,254,691,000** | **52,888,291,000** |

**Kiambatanisho Nam. 9A: Mradi wa Usimamizi wa shughuli za Uvuvi wa kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOfish)**

| |
|---|
| Gharama za mradi: **Kwa mwaka 2020/2021** Mradi uliombewa **7,824,935,033/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo (Benki ya Dunia). Hadi kufikia Machi, 2021 mradi ulipatiwa **TZS. 4,287,240,303/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo na hakuna fedha zilizopatikana kutoka SMZ |
| **Lengo Kuu la mradi**: Kuimarisha usimamaizi wa shughuli za uvuvi |
| **Malengo ya mwaka: 2020/2021**<br>• Kutoa taaluma na Usimamizi wa uvuvi wa kipaumbele kwa kufanya mamabo yafuatayo:<br>– Kuendelea kutayarisha mpango Mkuu wa Uvuvi na Kupitia ya Sheria ya Uvuvi ya 2010.<br>– Kuendelea kusomesha wanafunzi kwa fani za uvuvi 5 MSc na 2 PhD na kufanya tafiti za uvuvi<br>– Kukuza mfumo wa takwimu za uvuvi na kutayarisha rasimu ya sensa ya Uvuvi.<br>– Kukuza usimamizi wa uvuvi katika ngazi ya Taifa kwa kutayarisha Mipango ya usimamizi wa uvuvi uliopewa kipaumbe (Pweza, Samaki wa kwenye Matumbawe, Jamii ya madagaa na Jamii ya jodari),<br>– Kukuza usimamizi katika ngazi ya jamii kwa kutayarisha na kupitia Mipango ya Usimamizi wa maeneo ya hifadhi (GMPs) ikiwemo 3 ni mapitio na 2 mpya, Kusimamia mikutano ya kamati za uvuvi na maeneo ya hifadhi na Kutoa mafunzo na kutayarisha Taratibu za ushirikishaji wa jamii katika shughuli za usimamizi<br>– Kukuza doria ya gharama nafuu nafuu kwa kuendeleza kufanya doria katika maeneo ya hifadhi<br>– Kukuza utendaji wa taasisi na mali umma kwa Kutoa maunzo ya muda mfupi kwa watendaji, kukamilisha jengo na ununuzi wa samani kwa taasisi ya tafiti za uvuvi na kuweka maboya katika maeneo ya hifadhi<br>• Kukuza biashara na mazingira ya uwekezaji ikiwemo Kuongeza fursa kwa uvuvi wa kipaumbele na kuongeza thamani kwa bidhaa za uvuvi kwa kuendeleza na kuanzisha vya vikundi vya uvuvi vya kuweka |

| |
|---|
| na kukopa, Kusaidia kutoa vifaa vya kulimia mwani na kufanya ukarabati wa masoko ya Samaki ya Nungwi na Tumbe.<br>• Kuratibu shughuli za mradi wa mradi kwa kusimamia shughuli za utekelezaji na kutayarisha mpango wa ufuatiliaji na Tathmini |
| **Utekelezaji wa Malengo**<br>• Kutoa taaluma na Usimamizi wa uvuvi wa kipaumbele<br>– Mkataba mpya kwa ajili ya kazi ya ziada juu ya kutayarsiaha rasimu ya Mpango mkuu wa uvuvi uko katika hatua ya majadiliano na mshauri elekezi, Mapitio ya sheria ya Uvuvi numb 7, 2010 yanaendelea kwa kuwashirkisha wadau mbalimbali (Jamii na Taasisi),<br>– Wanafunzi 5 MSc na 2 PhD wanaendelea na mafunzo yao ya uvuvi na Kazi za tafiti bado zinaendelea katika maeneo husika<br>– Mfumo wa takwimu za uvuvi umeshakamilika na hivi sasa uko katika hatua za kuingiza taarifa zilizokusudiwa na Rasimu ya sensa ya uvuvi mwaka 2020 imetayarishwa<br>– Rasimu za Mipango ya usimamizi wa uvuvi uliopewa kipaumbe (Pweza, Samaki wa kwenye Matumbawe, Jamii ya madagaa na Jamii ya jodari) zimewasilishwa Idarani kwa hatua zinazoendelea.<br>– Rasimu za mapitio na matayarisho ya Mipango ya Usimamizi wa maeneo ya hifadhi (GMPs) ikiwemo 3 ni mapitio na 2 mpya imewasilishwa idarani kwa hatua zinazoendelea, Mfunzao yametolewa na rasimu ya Taratibu za ushirikishaji wa jamii katika shughuli za usimamizi zimewasilishwa<br>– Doria mbalimbali zinaendelea kufanyika katika maeneo ya hifadhi<br>– Wafanyakazi 9 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi, Jengo na ununuzi wa samani kwa taasisi ya tafiti za uvuvi umekamilika na rasimu ya taarifa ya uchambuzi yakinifua juu ya uwekaji maboya katika maeneo ya hifadhi imepitiwa kwa kushirikianana na wataalamu kutoka Bandari<br>• Jumla ya vikundi 110 vimehamasihswa na kupatiwa mafunzo ya kuweka na kukopa kwa ajili ya biashara inayohusiana na shughuli za uvuvi, jumla ya vihori 500 ya kubebea mwani vimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, ukarabati wa masoko ya Samaki ya Nungwi na Tumbe umekamilika. |

- Rasimu ya mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini umetayarishwa na kuwasilishwa Idarani kwa hatua zinazofuata

**Gharama kwa mwaka 2021/2022.** Mradi unaombewa **TZS. 4,443,487,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo (Benki ya Dunia**)**

**Malengo kwa mwaka 2021/2022**

- Kutoa taaluma na Usimamizi wa uvuvi wa kipaumbele
  - Kukamilisha utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Uvuvi na mapitio ya taratibu za sheria ya Uvuvi numb 7, 2010
  - Kuendelea kuwalipia wanafunzi 5 MSc na 2 PhD katika mafunzo yao ya uvuvi na Kuendelea na tafiti katika maeneo husika
  - Kufuatilia uchukuwaji wa taakwimu sahihi na Kufanya mikutano ya mrejesho wa wadau (Jamii)
  - Kukamilisha Mipango ya usimamizi wa uvuvi uliopewa kipaumbe (Pweza, Samaki wa kwenye Matumbawe, Jamii ya madagaa na Jamii ya jodari) kwa kuthibitishwa.
  - Kukamilisha na kuthibitisha mapitio na matayarisho ya Mipango ya Usimamizi wa maeneo ya hifadhi (GMPs) ikiwemo 3 ni mapitio na 2 mpya, Kuendelea na Mfunzao kwa jamii na kuthibitishwa kwa Taratibu za ushirikishaji wa jamii katika shughuli za usimamizi
  - Kuendelea kufanya doria katika katika maeneo ya hifadhi
  - Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 10 Kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya taasisi ya tafiti za uvuvi na Kununua na kuweka maboya katika maeneo ya hifadhi.
- Kuendela na kuhamasisha na kupatiwa mafunzo ya kuweka na kukopa kwa ajili ya biashara inayohusiana na shughuli za uvuvi.
- Kutekeleza shughuli za Ufuatiliaji na Tathminiza Mradi

## Kiambatanisho Nam. 9 B: Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki Malindi

| |
|---|
| Gharama za mradi: **Kwa mwaka 2020/2021** Mradi uliombewa **TSH. 3,797,816,200** kutoka **SMZ** na **TSH. 23,281,703,800** kutoka washirika wa maendeleo (JICA) zimetengwa kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha mwaka wa fedha **2020/2021**. Hadi kufikia Machi, 2021 mradi ulipatiwa **TZS. 10,110,529,550/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo na hakuna fedha zilizopatikana kutoka SMZ |
| **Lengo Kuu la mradi**: Kuwawezesha wadau wanaotumia diko la Malindi kuuza na kununua samaki wao wakiwa salama kiafya pamoja na kuwepo mazingira mazuri ya kuweka vyombo vya uvuvi na biashara kwa wavuvi, wachuuzi, madalali, wauzaji wadogo wadogo na wanunuzi |
| **Malengo ya mwaka: 2020/2021**<br>• Ujenzi wa Diko na soko la samaki kwa fedha za JICA (Lot1)<br>– Kujenga wa maeneo ya kuegeshea vyombo vya uvuvi<br>– Kujenga jengo la biashara na ofisi za usimamizi<br>– Utayarishaji wa Miongozo ya Usimamizi na Uendeshaji<br>• Ujenzi wa Diko na soko la samaki kwa fedha za SMZ (Lot2)<br>– Kukarabati wa soko la zamani<br>– Kujenga vyoo, Sehemu ya kuhifadhia genereta na Kibanda cha mlinzi, |

- Sakafu ya nje, mitaro ya maji machafu na maeneo ya kuegeshea vyombo vya juu

**Utekelezaji wa Malengo**

- Ujenzi wa Diko na soko la samaki kwa fedha za JICA
- Ujenzi wa maeneo ya kuegeshea vyombo vya uvuvi umekamilika kwa 95% kazi iliyobakia ni kuweka F*ender* za kuegeshea boti
- Mpango wa endeshaji umeshakamilika kazi iliyobakia ni kukamilisha mpango wa fedha na kanuni za diko na soko la Samaki Malindi
- Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshakubaliana na mkandarasi RINKAI NISSAN Cosntruction ltd kujenga kwa kutumia fedha za SMZ, aidha, ujenzi huo unatarajiwa kuendelea mwezi wa Jun 2021

**Gharama kwa mwaka 2021/2022** Mradi unaombewa **Jumla TZS 24,741,600,000 (TZS. 21,141,600,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo (JICA**) na TZS 3,600,000** kutoka **SMZ).**

**Malengo kwa mwaka 2021/2022**

- Kuendelea Ujenzi wa Lot 1 kwa
  - Kumalizia ujenzi wa eneo la kuegesha vyombo vikubwa kwa kwa kuweka vifaa vya kufungia vyombo (Fender) na kusafisha eneo kwa kuondoa pile za muda na mchanga
  - Kukamilisha ujenzi wa mashimo ya maji machafu (septic tanks)
  - Kujenga jengo la kufanyia biashara na ofisi za uendeshaji
  - Kukamilisha kutayarisha mipango ya uendeshaji (Fedha na Kanuni)
- Kuanza ujenzi wa Lot 2 kwa kufanya mambo yafuatayo.
  - Kukarabati wa soko la zamani,
  - Kujenga vyoo, Sehemu ya kuhifadhia genereta na Kibanda cha mlinzi,
  - Sakafu ya nje, mitaro ya maji machafu na maeneo ya kuegeshea vyombo vya juu

- Majukumu mengine ya SMZ
  - Kufanya ufuatiliaji wa hali ya kimazingira (Environmental Monitoring) katika eneo la ujenzi
  - Kufanya ufuatiliaji wa mambo ya kale (Archaeological survey) katika eneo la ujenzi
  - Kuweka Mtambo wabarafu chenga na Jenereta
  - Kufanya manunuzi wa vifaa vya samani
  - Kufanya manunuzi na uwekaji wa viyoyozi ndani ya soko jipya
  - Kufanya manunuzi ya vifaa vya vyengine vya soko (Boksi za Samaki, Majokofu, pampu ya kusafishia, Matangi ya maji, vibao vya kuchakatia Samaki, meza za kuhamisha,

**Kiambatanisho Nam. 9 C: Mradi kutotolea Vifaranga vya Samaki, Kaa na Majongoo bahari (*Marine Hatchery*)**

| |
|---|
| Gharama za mradi: **Kwa mwaka 2020/2021** Mradi uliombewa **TSH. 736,479,000** kutoka washirika wa maendeleo (KOICA) zimetengwa kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha mwaka wa fedha **2020/2021**. Hadi kufikia Machi, 2021 hakuna fedha iliyotolewa. |
| **Lengo Kuu la mradi**: Kuimarisha ufugaji wa Samaki na mazao mengine ya bahari |
| **Malengo ya mwaka: 2020/2021**<br>• Kuzalisha vifaranga vya Majongoo bahari 50,000 na Kaa 50,000<br>• Kutoa elimu kwa wafugaji 95 wa mazao ya baharini Unguja na Pemba<br>• Kuimarisha miundombinu ya ufugaji na kusambaza vifaranga vya Kaa na Majongoo bahari ikiwemo kuwapatia mafunzo wafanyakazi 7 wa Kituo cha kutotolea vifaranga vya Samaki, Kaa na Majongoo bahari, Beit-el-Ras. |
| **Utekelezaji wa Malengo**<br>• Kwa sababu ya maradhi ya COVID-19 KOICA haikuweza kufadhili mradi huu kama ilivyoahidi. Hatahivyo, kazi chache zilitekelezwa na watendaji wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi<br>• Jumla ya vifaranga vya Majongoo 37,500 vimezalishwa. Aidha, kambare 16,364 na Sato 12,970 walizalishwa na kugawiwa kwa wananchi<br>• Jumla ya wanajamii 350 wamepatiwa mafunzo yanayohusiana na ufugaji wa Samaki na mazao mengine ya baharini |

mpya za ukulima wa mwani, kuongeza thamani na mikutano mbalimbali, kufanya mikutano na kuwawezesha wakulima wa mwani kuongeza thamani pamoja na kufanya upembuzi wa shughuli za kilimo cha mwani na ufugaji wa Samaki katika maeneo ya hifadhi

- Kuwezesha ukulima wa mwani na wafugaji wa samaki kwa kuwapa vifaa na utaalamu ikiwemo kuanzisha vitalu vya *tissue culture* na mashamba darasa na kuwajengea uwezo pamoja na kuwawezesha kutayarisha vitalu vya mwani
- Kupunguza kupotea kwa ubora wa mazao (Samaki na mwani) kwa kujenga mtambo wa barafu na uendeshaji wake
- Kukuza usarifu wa mazao kwa kujenga makaushiyo ya jua na kununua makaushio ya umeme kwa dagaa, kununua mtambo wa kusarifu mwani, kunua magari ya kusafirishia Samaki
- Kuanzisha ufugaji wa mashamba darasa ya Samaki Unguja na Pemba
- Kuanzisha na kuendeleza makongamano ya kijinsia na lishe ikiwemo kutoa elimu ya lishe na uhamasishaji
- Kuratibu shughuli za utekelezaji kwa kuendesha mikutano, kununua vyombo vya usafiri, Ufuatiliaji na tathmini, kufanya uchambuzi wa awali, na matumizi ya kuendeshea ofisi ya kawaida

**Kiambatisho Nam 9D: Mradi wa Kuimarisha Uvuvi na Kilimo (IFAD)**

| |
|---|
| Gharama za mradi: **Kwa mwaka 2020/2021** Mradi ulikuwa katika hatua za matayarisho na hayakuombewa pesa kwenye bajeti. Mradi huu, unatarajiwa kutekelezwa na washirika wa maendeleo IFAD. |
| **Lengo Kuu la mradi**: ni "kuongeza tija endelevu, uthabiti, faida na biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki", kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. |
| **Malengo ya mwaka: 2020/2021**<br>• Kutayarisha mradi kwa kushirikiana na tanzanaia bara |
| **Utekelezaji wa Malengo**<br>• Mikutano mbalimbali ilifanyika katika kutayarisha mradi ikiwemo kutayarisho makubaliano na kusainiwa na pande zote mbili (mshirika wa maendeleo (IFDA na serikali ya Muungano wa Tanzania), kupanga mikakati ya utekelezaji pamoja na kutayarisha bajeti |
| **Gharama kwa mwaka 2021/2022.** Mradi unaombewa **TZS. 10,506,456,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo (Benki ya Dunia**)** |
| **Malengo kwa mwaka 2021/2022**<br>• Kuanzisha uvuvi wa ubia na sekta binafsi kwa kununua meli 2 za uvuvi, kutayarisha mfumo wa uvuvi wa kibiashara, kutayarisha mfumo wa ubia na uchambuzi yakinifu wa uendeshaji<br>• Kufanya upembuzi wa kimazingira kwa meli za uvuvi wa maji ya kina kirefu, viwanda vya usarifu na chumba cha baridi<br>• Kutoa elimu na kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa kutayarisha nyaraka za kufundishia juu ya mbinu |

mpya za ukulima wa mwani, kuongeza thamani na mikutano mbalimbali, kufanya mikutano na kuwawezesha wakulima wa mwani kuongeza thamani pamoja na kufanya upembuzi wa shughuli za kilimo cha mwani na ufugaji wa Samaki katika maeneo ya hifadhi

- Kuwezesha ukulima wa mwani na wafugaji wa samaki kwa kuwapa vifaa na utaalamu ikiwemo kuanzisha vitalu vya *tissue culture* na mashamba darasa na kuwajengea uwezo pamoja na kuwawezesha kutayarisha vitalu vya mwani
- Kupunguza kupotea kwa ubora wa mazao (Samaki na mwani) kwa kujenga mtambo wa barafu na uendeshaji wake
- Kukuza usarifu wa mazao kwa kujenga makaushiyo ya jua na kununua makaushio ya umeme kwa dagaa, kununua mtambo wa kusarifu mwani, kunua magari ya kusafirishia Samaki
- Kuanzisha ufugaji wa mashamba darasa ya Samaki Unguja na Pemba
- Kuanzisha na kuendeleza makongamano ya kijinsia na lishe ikiwemo kutoa elimu ya lishe na uhamasishaji
- Kuratibu shughuli za utekelezaji kwa kuendesha mikutano, kununua vyombo vya usafiri, Ufuatiliaji na tathmini, kufanya uchambuzi wa awali, na matumizi ya kuendeshea ofisi ya kawaida

## Kiambatisho Nam. 9E: Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa

| JINA LAMRADI | Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu Dagaa |
|---|---|
| MUDA | Julai 2021 – June 2022 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 12,497,446,120** |
| LENGO KUU | Kujenga kiwanda cha kusarifu Dagaa maeneo ya Mkokotoni Fungu Refu |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2021/2022 | Jumla ya **TZS 4,277,607,000** zimetengwa kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2021/2022:<br>1) Kutangaza zabuni kwa ajili ya kutafuta Mkandarasi wa ujenzi wa kiwanda<br>2) Kuaza ujezi wa kiwanda kwa hatua za awali<br>3) Kutafuta hati miliki ya eneo | |

## Kiambatisho Nam 9F: Mradi wa Kuanzisha Mashamba na Kufuga Samaki

| JINA LA MRADI | Kuanzisha shamba la samaki |
|---|---|
| MUDA | 2021 – 2024 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 23,000,000,000** |
| LENGO KUU | Kuanzisha maabara ya kutotolea vifaranga vya samaki na kufuga katika mashamba yatakayojengwa baharini karibu na kisiwa cha Popo |
| FEDHA ZILIZOTENGWAKWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 | Jumla ya **TZS. 463,800,000** zimetengwa kutoka fedha za maendeleo za SMZ. |
| Malengo ya Mradi kwa mwaka wa fedha 2021/2022:<br>1) Kulipa fidia za mazao kwenye shamba linalotarajiwa kujengwa kiwanda<br>2) Kutafuta hati miliki ya eneo linalotaka kujengwa kiwanda<br>3) Kuratibu shughuli zote za uanzishwaji wa kiwanda<br>4) Kutafuta Mshauri elekezi kwa ajili ya michoro ya kiwanda<br>5) Kuanza ujenzi wa kiwanda. | |

**Kiambatisho Nam 9G: Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Usarifu na Uhifadhi wa Bidhaa za Samaki ZAFICO**

| JINA LA MRADI | Ujenzi wa kituo cha usarifu na uhifadhi wa bidhaa za samaki ZAFICO |
|---|---|
| MUDA | Mwaka 2021- 2022 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 16,774,680,882** |
| LENGO KUU | Kujenga kiwanda cha kuchakata na kusarifu minofu ya samaki Malindi Zanzibar. |
| FEDHA ZILIZOTENGWA KWA MWAKA 2021/2022 | Jumla ya **TZS 8,292,193,000** zimetengwa kutoka fedha za miradi ya maendeleo SMZ. |
| Malengo ya mradi:<br>1) Kuangusha jengo liliopo katika eneo kwa sasa<br>2) Kutangaza zabuni ya ujenzi wa kiwanda<br>3) Kuanza kwa ujenzi wa Kiwanda | |